Kukata Tamaa

Na tuendelee kusimama tunapoinamisha vichwa vyetu.

Bwana Yesu, kwa kweli tunaamini tu. Umetwambia tuamini tu, nasi tunaamini sasa. Nasi tunakupa shukrani na sifa kwa yale tuliyokwisha kusikia na kuona, ambayo yanaitia nanga imani yetu. Jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya nafasi nyingine ya kuja kuwahudumia wale walio wahitaji. Sasa ninakuomba, Mungu, ututimizie haja zetu usiku wa leo kulingana na ahadi Yako. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

2 Tuna furaha sana usiku wa leo kwa ajili ya majaliwa haya ya kurudi maskanini tena, kwenye—kwenye . . . na Injili ya Bwana Yesu aliyefufuka. Nami nilichelewa kidogo tu. Nilikuwa na jambo maalum la dharura kutoka Michigan sasa hivi. Na Bwana alifanya jambo la ajabu wakati uo huo kwa ajili ya mwanamke huyo. Jamani, jinsi anavyojua kila kitu na kuliweka ninii tu . . . Haikubidi kumwambia; Yeye anajua, Yeye anajua tu ni kitu gani. Na kwa hiyo tunashukuru sana. Watu waliendesha magari siku nzima wapate kuja hapa. Na, basi, tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo. Sasa, msisahau ninii . . .

Kanda inarekodi? [Ndugu Neville anasema, "Hiyo ni swichi ya taa hapo."-Mh.] Loo, swichi ya taa. Sawa.

Msisahau i—ibada juma hili lijalo, Jumatano usiku, na Jumapili ijayo asubuhi, na Jumapili usiku. Kama mko hapa karibu, jirani zetu, ninajua bila shaka wangefurahia kuwa pamoja nanyi hapa.

Na sasa, niombeeni, ninaposhika safari ya kwenda mahali pengine, nami ninatarajia kurudi tena hivi karibuni.

3 Ninataka kuwashukuru ninyi nyote kwa wema wenu na kumbukumbu la yale mliyonitendea. Na ndugu fulani amenitumia hivi karibuni suti mpya kutoka kanisa dogo huko Georgia. Na—na hao watu . . . Ni ajabu kabisa. Nami ninataka kuwashukuru watu hao kutoka huko Kentucky, niliokuwa pamoja nao juma lililopita kwenye likizo. Na yote yale ambayo Bwana alitutendea kule, mkono mkubwa, wenye nguvu sana tulioouona, yale Yeye aliyofanya.

4 Sasa tunatarajia kuwaona tena hivi karibuni sana, mara tu nitakaporudi huku, nikienda huko New York kwa ajili ya ule mkutano. Ni kwenye Kanisa la Stone kwa Ndugu Vick, kuanzia, ninaamini ni Novemba 12. Nasi tutakuwa tumerudi hapa, siku chache kabla ya wakati huo.

Ndipo tutapitia hapa tena, tukienda hu—huko Shreveport, Louisiana, pamoja na Ndugu Jack Moore. Hiyo ni kwenye ninii ya Shukruni, juma la Shukrani, tuwe kule Shreveport.

Liko kwenye ubao wa matangazo, nafikiri, kule nyuma kwenye matangazo.

5 Halafu basi tunatumainia kuwa pamoja na baadhi ya marafiki wa Kusini baada ya Krismasi. Na tutakuwako huko Phoenix Januari. Halafu tena tunaangojea wito wa kwenda nchi za ng'ambo, ili tuweze kuitayarisha mikutano ya nchi za ng'ambo. Wanaishughulikia sasa, mwezi huu uliopita, Ndugu Borders, wakiandikiana barua, kwa sababu ya ziara ya kuzunguka ulimwengu mzima itakayoanza mara tu tutakapoweza kuitayarisha, lakini itatubidi kungojea hali ya mambo iwe sawa.

6 Umati wa watu ni mkubwa sana kule, hatuwezi kuuweka ndani ya majengo; inatubidi tu kuwaweka nje uwanjani. Halafu basi wakati mwingine wanafikia, karibu mtu hawezi kuamini idadi yao, wakati mwingine wanafikia laki tano. Hiyo ni watu nusu milioni katika mkutano mmoja, si idadi ya wangapi wanaohudhuria mkutano katika siku kadha, lakini katika kusanyiko moja. Unajua, kwa kawaida wainjilisti huhesabu ni watu wangapi waliohudhuria katika majuma sita. Unaona? Lakini sisi tu—tunahesabu ni wangapi waliopo siku hiyo, wakati huo mmoja. Na kwa hiyo wakati mwingine hakuna mahali pa kuwaketisha, wajua, inawabidi tu kuwaketisha chini.

Na inatubidi kwenda misimu ambayo haina mvua na mvua nyingi. Na maskini watu hao wanaketi kule nje . . . Nimewaona wanawake wameketi huko nje huku nywele zao zinaning'inia chini, watu waliovalia vizuri, na wa—wanaketi tu pale kwenye mvua hiyo siku nzima. Wanaketi pale tu, nayo inamwagika kwa wingi tu, na kunguruma, na umeme, na dhoruba zinavuma, nao wanaegemeana mmoja kwa mwingine namna hiyo, wakiketi papo hapo, wanangojea mpaka utakapokuja kuwaombea. Unaona? Sasa, unajua Mungu huheshimu imani kama hiyo. Anaiheshimu.

7 Huna budi kufanya jambo fulani kusudi Mungu aliheshimu. Unaona? Unamwonyesha. Watu ambao wanapewa kila kitu kwa urahisi sana, kwa kawaida wao hawaninii . . . Wao—wao hawafanyi jambo lo lote kwa ajili yake, unaona. Huna budi kuninii . . . Karama ni bure, hiyo ni kweli, lakini huna budi—huna budi kuninii . . .

8 Inaonekana namna hiyo, unajua, kama vile wasemavyo, "Kama ulizaliwa ukiwa na kijiko cha fedha," mmesikia jambo hilo, "hukithamini." Lakini inapokubidi kukifanyia kazi, unathamini thamani yake.

9 Sasa, ninyi watu kwenye kanda humo ndani, laiti—laiti . . . Nafikiri sasa mimi . . .

Asubuhi ya leo, ujumbe wa asubuhi ya leo ulikuwa, kwangu mimi, Ujumbe wa kipeo cha huduma yangu yote; asubuhi ya leo, unaona, Ujumbe wa kipeo cha huduma yangu yote. Siku

moja nitawaambia jinsi nilivyoupata. Nami ninajua ya kwamba kila kitu kimetenda kazi kwa miezi na miezi na miezi, kuelekea kwenye Ujumbe huo mmoja, ukisogea kuja mahali hapo. Huo ulikuwa ndio wakati wake wa kutia kifuniko, unaona. Na ni ninii . . .

10 Sasa nina hakika, ama ninatumaini, ya kwamba mlielewa kwamba Ishara ilimaanisha nini. Mnaona? Ile Ishara ni dalili ya kwamba Damu imepakwa. Ya kwamba, ile gharama ambayo inatakiwa, imeagizwa na Mungu, Yesu alilipa gharama hiyo kwa kumwaga Damu Yake Mwenyewe. Alifanya jambo hilo. Ndipo, kutoka katika uhai Wake akaja Roho Mtakatifu. Na wakati unapopakwa hiyo Damu, Roho Mtakatifu ni Ishara ya kwamba gharama yake imelipwa; Mungu amekupokea, na hiyo ndiyo Ishara. Kumbukeni, hiyo ndiyo Ishara. Sasa, kuna watu wengi ambao hawaninii, ha—hawajui hiyo Ishara ni kitu gani, unaona. Na inakubidi kufanya kana kwamba hakuna mtu anayeijua, unaona, ili kwamba wote wataipata.

11 Ni kama tu kuhubiri wokovu, inatubidi kuhubiri wokovu kama kwamba kila mtu, ni kwa ajili ya kila mtu, ambapo, tunajua si wa kila mtu. Inatubidi kuhubiri uponyaji wa Kiungu kwa kila mtu, hata hivyo tunajua si wa kila mtu. Mnaona? Yesu alikuja kuwaokoa wale waliokuwa katika Kitabu cha Ukombozi kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Yeye alikuja tu kuwaokoa hao. Kwamba hao ni akina nani, sijui. Unaona? Lakini wewe . . . Hakuna mtu anayeweza kuwa na imani isipokuwa useme ni ya kila mtu; na ni ya kila mtu, hakuna mtu anayeweza kuja isipokuwa wameitwa na Mungu. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo kuna watu wengi ambao hawataokolewa. Tunajua kuhusu jambo hilo. Wao, vema, Mungu alijua kwamba kabla ya ulimwengu haujaanza, ya kwamba hawangeokolewa.

12 Kuna wengi ambao hawataponywa, unaona, wengi hawataponywa. Hawawezi tu, hawawezi tu kulielewa jambo hilo. Hawajui ni nini. Wengi wataponywa. Lakini tunalihubiri kwamba ni wa kila mtu, kwa sababu hatujui mtu huyo ni nani; hatujui tu. Lakini hilo ni kwa atakaye, lakini watu wengine hawawezi kamwe kuipokea imani hiyo.

13 Sasa, na ni jambo lile lile juu ya Ishara hii. Ile Ishara, tumezungumza juu ya Ishara wakati wote, lakini sasa ni kudhihirishwa kwa Ishara. Unaona?

14 Sasa, wakati mwingine tunaichukua. Waluteri waliichukulia ni, "Kulikubali Neno; kumkubali Kristo kama Mwokozi wako binafsi." Wamethodisti walisema, "Unapofurahi vya kutosha kupaza sauti, Hilo Ndiye." Wapentekoste wanasema, "Nena kwa lugha, basi umempata." Nasi tunaona ya kwamba yote hayo ni makosa. Unaona?

Ishara ni Ishara. Ni wewe pamoja na Kristo kama watu mlio kitu kimoja. Unaona? Ni Roho Mtakatifu, Uzima Wake ndani

yako, akifanya ninii yake—akiishi Maisha Ya—Yake Mwenyewe ndani yako. Na ni kwa ajili ya matajiri, maskini, ama kwa ye yote atakayempokea Huyo. Sasa kumbuka, Ishara ni kile wewe . . .

15 Unaenda kwenye idara ya reli na unajinunulia tikiti. Kuna bei yake, gharama zake. Tuseme iligharimu senti hamsini kupanda basi hi—hili, ama gari la moshi, kutoka hapa mpaka—mpaka Charleston, Indiana, inagharimu senti hamsini. Vema, sasa, kampuni hiyo hutoa tikiti ili kwamba . . . Unaona? Sasa, jambo la wewe kufanya, unashuka unaenda kule na mtu fulani anakununulia tikiti, senti hamsini. Wanakupa ishara inayokupa haki kuwa kwenye gari hilo la moshi mpaka mwisho wa safari ya tikiti, po pote gari hilo la moshi linakoenda. Unaona? Inakupa . . . Hiyo ni ishara.

16 Sasa, katika jambo hili, damu ndiyo iliyokuwa ishara. Kiuhalisi ilibidi ipakwe yenyewe, kwa sababu wao walikuwa na na kemia peke yake, kwa maana ilikuwa ni damu ya mwana-kondoo, mnyama, damu ya mwana-kondoo. Kwa hiyo ule uhai uliokuwa katika ile damu, uhai huo uliotoka, kwa hiyo damu ulimwagika. Unaona? Uhai ulitoka, lakini haukuweza kumrudia mwamini, kwa maana ni wa mnyama. Lakini ulinena tu juu ya dhamiri njema, kwamba kuna Mtu aliyekuwa anakuja, Dhabihu kamilifu.

Na, kuifanya Hiyo kuwa kamilifu, Hakimu mwenyewe, Mungu wa Mbinguni, alifanyika Dhabihu; Hakimu, Waamuzi, na Wakili. Unaona? Yeye alifanyika Dhabihu. Na ndipo Uhai Wake ulipotoka, ambao ulikuwa ni Mungu . . . Na neno hapo, mahali linapokuja, "Nami nitawapa Uzima wa Milele." Sasa, katika Kiyunani . . . Ninajua ninazungumza na wataalamu. Ninaona wawili ama watatu. Unaona? Nami . . . Na neno hilo katika Kiyunani pale, ni Zoe. Z-o-e, katika Kiyunani, ambalo linamaanisha, "Uzima wa Mungu Mwenyewe." "Nami nitawapa *Zoe*, Uzima Wangu Mwenyewe." Kristo na Mungu walikuwa ni Mmoja.

17 Basi, Uzima ule uliokuwa katika Kristo ni Roho Mtakatifu, si Nafsi ya tatu; lakini Nafsi ile ile, katika mfano wa Roho Mtakatifu, akija juu yako, kama Ishara ya kwamba uzima wako na nauli yako vimelipiwa, umekubalika. Mpaka ishara hiyo itakapokuja, huruhusiwi kwenye barabara kuu, huruhusiwi kuninii . . . kuninii—kusafiri kwenye shirika la mabasi; huruhusiwi kuingia mpaka uweze kuonyesha ishara hii, na ishara hiyo ndiyo nauli yako. Na sasa, Hiyo inaonyesha ya kwamba ile Damu imekwisha kumwagwagika na umepakwa, umelipiwa bei, nawe una Ishara ya kwamba umepakwa ile Damu na umekubalika. Mmeelewa sasa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Loo, jamani! Loo!

18 Sasa—sasa, si thibitisho fulani tu. Unaona? Unasema, "Ndugu Branham," ninalihisi niani mwenu, mnaona, "nitajuaje?"

Angalia, ulichokuwa, na ulicho sasa? Hivyo ndivyo unavyojua. Unaona? Ulikuwa nini kabla Ishara hii haijawekwa? Wewe ni nini baada ya Hiyo kuwekwa? Shauku yako ilikuwa ni nini hapo kabla, na shauku zako ni nini baadaye? Ndipo unajua kama ile Ishara imewekwa ama huijawekwa. Na mambo haya mengine yanaambatana tu na Hiyo moja kwa moja. Unaona?

19 Si—si kule kuzungumza juu ya jambo hilo, na kusema, "Lugha ndiyo ushahidi." Sasa, nitaninii, nitanunua jozi ya viatu, kilimi chake sicho kiatu hicho. Kinakuja tu na kiatu hicho, unaona. Huja tu na kiatu. Unaona? Basi, na Ishara ni vile vile. Ile Ishara ni Kristo. Lakini kunena kwa lugha, na kutoa pepo, na kufanya mambo hayo yote, na kuhubiri, na cho chote kile, ni ushahidi ya kwamba Ipo, kweli, lakini sininii—Hiyo siyo. Mnaona, ni kipawa Chake. Kama nilikwambia ya kwamba . . .

20 Unasema, "Ni—ninakutaka wewe, Ndugu Branham," na mimi nitoe zawadi nikupe, unaona. Vema, hiyo si mimi, hiyo ni zawadi yangu.

Lugha ni kipawa cha Roho Mtakatifu, si Roho Mtakatifu; kipawa cha Roho Mtakatifu.

21 Na ibilisi anaweza kuiga cho chote cha mambo hayo, lakini hawezi kuwa Roho Mtakatifu. Unaona? Yeye anaweza kuiga vipawa hivi, lakini hawezi kuwa Roho Mtakatifu.

Na Roho Mtakatifu ni Ishara ya kwamba ile Damu imepakwa, kwa maana Yeye anafuata Damu sikuzote katika Kitabu cha Ukombozi. Unaona jambo hilo? Hilo lilikuwa ndilo kusudi la Yeye kuja. Hilo ndilo Yeye alilofuata katika kila wakati. Kila wakati ameliandama hilo, kuhakikisha ya kwamba limetekelezwa, nao hawangeweza kukamilishwa bila ya sisi. Na sasa Roho Mtatifu mzima analizuru Kanisa, akijifanya Mungu katika mwili wa mwanadamu; kama alivyofanya kabla ya Sodoma, kule kuteketezwa pale, ambako kulikuwa ni mfano. Halafu, Ibrahimu, Yeye alimtokea.

22 Na mambo yote ambayo hajafanya katika miaka yote, katika zile nyakati, katika zile nyakati za kanisa, Yeye anayafanya sasa. Rudini kwenye Neno, kwa sababu jumbe na jumbe na jumbe hazina budi kuishia katika Neno lote. Na katika siku za mwisho, ile Mihuri Saba ikifunguliwa, ilikuwa ikusanye kila kipengee kilichosalia ndani yake, na kufanyiza kitu hicho chote katika mwili mmoja mkubwa wa Bibi-arusi, ili kwamba hao walioishi huko nyuma hawakuwa wakamilifu mpaka Kanisa hili likamilishwe, kundi hili la Bibi-arusi katika siku za mwisho, kuwaingiza ndani, na sisi sote pamoja tunyakuliwe. Unaona?

23 Ile Ishara, Yesu Kristo, Roho Mtakatifu, yuko miongoni mwetu. Tunapaswa kuheshimu jambo hilo. Ha—ha—ha—hatuwezi kujinyenyekeza vya kutosha. Kuvua viatu vyako, ama kupiga magoti yako, hakutaliondoa jambo hilo; haku—

hakutaridhisha, hakutatutosha; ila maisha yanayozaa tunda la Roho!

24 Sasa, tunda la Roho ni nini? Unaona? Upendo, furaha, amani.

25 Mnakumbuka asubuhi ya leo? Yale matayarisho, akamtuma mjumbe na Ujumbe. Jambo linalofuatia alilofanya, baada ya kumtuma mjumbe na Ujumbe, Yeye alituma Nguzo ya Moto kwa ajili ya thibitisho. Jambo lililofuata lilikuwa, baada ya hilo, kund-. . .ama ni faraja. Unaona? Ulijua jambo hilo lilikuwa ni kweli, ukapata amani. Tuna amani na Mungu, katika Bwana Yesu Kristo. Unaona?

26 Sasa usiku wa leo tutawaombea wagonjwa, na ninafikiri wao wana ushirika. Je! m—mtakuwa na ubatizo, ibada ya ubatizo? [Ndugu Neville anasema, "La."—Mh.] Ni ushirika tu, ushirika. Nasi tunataka mngojee ushirika.

27 Na katika—katika dakika thelathini na tano ama arobaini tunakusudia kuwa tumemaliza na kuwa tayari kwa ajili ya ushirika. Na sasa, kesho ni siku ya Wafanya Kazi, kwa hiyo kwa namna fulani mnaweza mkapumzika. Sasa, nilisema hilo lilikuwa ndilo kusudi letu, mnaona. Hatujui ni wakati gani. Ninataka kuhakikisha nimesahihisha jambo hilo.

28 Sasa, asubuhi ya leo niliwaambia, kwa kuwa sikuwa pamoja nanyi, ni—ninafikiri tulikuwa na Ujumbe mwingine wa masaa mawili ama matatu asubuni ya leo. Lakini—lakini ni—niliuanza tu, nami nikafikiri ningeendelea tu nao usiku wa leo, lakini ulikuwa ni mzuri mno. Sijui kama watu waliupata ama hawakuupata. Ninatumaini wanaupata, kila mahali. Nami ninatumaini kulikuwako na kanda nzuri za huo, ili iweze kutangazwa, kujulikana, ya kwamba ninaamini, kati ya Jumbe zote ambazo niliwahi kuleta, huo kabisa ulitoka kwa Mungu, nje ya ninii. . .Bila shaka, agizo la kawaida, kama ile Mihuri Saba na kadhalika, hiyo ilikuwa ni moja kwa moja Neno la Mungu. Ninazungumza juu ya Ujumbe wa kuhubiri; ninaamini ya kwamba huo ulikuwa ndio wenyewe, unaona, ule—ule, ule unaotakiwa kufuatia ile Mihuri Saba.

29 Sasa angalia kile kilichokuja baada ya ile Mihuri Saba: ule muungano wa watu, ishara zilizounganika, kimulimuli chekukundu katika siku za mwisho, ishara ya wanawake kuzidi kuwa warembo, na wanaume, kile wangefanya. Ishara hizi zote za Roho Mtakatifu akituongoza, kisha kurudi moja kwa moja hapa kwenye kifuniko cha Jumbe hizo zote tangu ile Mihuri Saba. Zinafikia kwenye kifuniko chake katika kitu hiki kimoja, ile Ishara, ya kwamba tuko sawa, unaona, tujichunguze tu na tuone kama tuko katika Imani.

30 Sasa, Bwana awabariki. Na sasa, kabla hatuja—kabla hatujafungua Biblia, kuwaombea wagonjwa. . . Tuliuliza asubuhi ya leo, ni wangapi walioombewa Jumapili iliyopita

usiku, ambao—ambao—ambao waliponywa, wameponywa tayari juma hili, na karibu kila mtu hapa aliinua mkono wake juu, hiyo ilikuwa kwenye mkutano wa Jumapili iliyopita usiku. Sasa, ni jambo fulani, mnalofahamu. Ni jambo fulani ambalo . . . Ni, ninashika jambo hili kwa ajili yangu binafsi.

31 Kulikuwa na mvulana mdogo, ambaye aliambiwa tu, alitoka Chicago, maskini Bibi . . . Ni yule mwanamke, Peckinpaugh, Peck- . . . Bibi Peckinpaugh kutoka—kutoka . . . Yeye ni dada mzuri sana Mkristo. Naye alimleta mtu fulani, m—mtoto, jinsi ninavyofahamu, mvulana mdogo ama kitu kama hicho, ambaye—ambaye . . . madaktari hata hawakujua anaumwa na nini. Mapafu yake yalikuwa mabovu sana, ama cho chote kile, hata—hata wao hawangeweza kufanya ninii . . . hawangeweza kumpeleka shuleni ama kitu kama hicho. Yeye alikuwa na hali mbaya, mgonjwa sana. Naye akasema, Roho Mtakatifu mara baada ya ule Ujumbe, akanena na mvulana huyo mdogo, na kumwita, akamwambia hali zake na kadhalika, na kutangaza kuponywa kwake.

Na juma hili akaenda, mama, ama wazazi, ama ye yote yule, alimrudisha kwa daktari, naye daktari akasema alikuwa na seti mya ya mapafu, unaona, mapafu mawili mapya. Na ninavyofahamu, ni kwamba—ni kwamba wazazi wake ama mtu fulani alipiga simu ya kutoka mbali, ama njia yo yote, kulifahamisha kusanyiko. Unaona? Sasa, Mungu, Muumba, anaweza kuumba seti ya mapafu.

32 Ni—ninaamini hakika ya kwamba tuko u—ukingoni mwa moja ya mambo makuu sana yaliyowahi kuwako duniani tangu siku za Bwana Yesu. Mnaona? Mnaona? Lakini sasa tunaweza tu kujulikana kama . . . Litakuwa ni nyenyekevu sana. Unaona? Unaona, kile mwanadamu anachoita *kikuu*, Mungu hukiita "chukizo." Lakini kile mwanadamu anachoita *kipumbavu*, Mungu hukiita "kikuu". Unaona? Kwa hiyo sasa angalia jambo hilo, unaona, litakuwa nyenyekevu sana hata hutakosa kamwe . . . hata utalikosa iwapo huna ile Ishara mle kulichunguzia, unaona. Unaona?

33 Ni nani angaliweza kuwazia ya kwamba milima ilikuwa ikirukaruka kama madume ya kondoo, na majani yalikuwa yanapiga makofi yao, wakati nabii alipokuja kutoka nyikani; jambo ambalo lilinenwa na Isaya, miaka elfu moja mia mbili . . . ama miaka mia saba na kumi na mbili hapo kabla. Akiwa na masharubu usoni mwake mwote, na kipande cha ngozi ya kondoo, hana hata mimbara ya kuhubiria, ametengwa kutoka katika makanisa yote, naye amesimama ukingoni mwa Yordani, akilia kwa sauti kuu, "Tubuni!" Na kuwaita watu kundi la "majoka," nyoka. Lakini hivyo ndivyo Mungu alivyosema, ya kwamba wakati atakapokuja, "milima itarukaruka kama ndama dume wadogo wa kondoo." Unaona? Wale wanyenyekevu waliona jambo hilo na wakafurahi.

34 Wangewezaje kuelewa ya kwamba ninii—ya kwamba Masihi mkuu, ambaye alitabiriwa tangu mwanzo kabisa wa kile Kitabu, katika Mwanzo, ya kwamba Yeye angekuja, Mwokozi? Dhabihu zote, na manabii wote, na kila kitu kilikuwa kimemwelekezea yeye kidole. Halafu basi wakati Yeye alipokuja, akidhaniwa kwamba ni mwana haramu; baba ambaye hata hakuwa amemwoa mama Yake, ilivyodhaniwa. Mnaona? Na mwanamke huyo alionekana ana mimba ya mtoto mchanga kabla wao hata hawajafunga ndoa. Na akatokea katika ninii sana, na kuzaliwa katika ninii ndo— ndogo . . . Vema, inasema banda la ng'ombe, katika Biblia. Lakini banda la ng'ombe katika siku hizo lilikuwa ni pango nyuma kwenye—kule nyuma katika ukuta. Niliona mahali kama hapo huko Arizona wakati mmoja, nilipokuwa nikiwinda. Kulikuwako na banda la ng'ombe kule nyuma chini ya genge la miamba. Na hivyo ndivyo Yesu alivyozaliwa, huko nyuma kwenye banda dogo la ng'ombe la magenge kwenye hori la kulia ng'ombe la manyasi makavu na majani makavu, katika kibanda cha ng'ombe, unaona, ambamo mlikuwamo na mifugo.

35 Naye alilelewa kama msaidizi wa seremala; na huyo angewezaje kuwa ndiye Yehova mwenye uwezo? Lakini alikuwa hivyo, mnaona. Alikuwa Ndiye. Unaona? Mtu wa kipekee sana. Lakini, loo, wakati alipokuwa mvulana tu, aliwashangaza makuhani kwa kulijua hilo Neno. Kwa sababu gani? Yeye alikuwa ni Neno. Unaona? Yeye alikuwa Neno.

Hakuandika kitabu kamwe. Kamwe hakuandika ninii—Yeye hakuandika hata neno moja. Neno pekee alilopata kuandika, nadhani, alilifutilia mbali, kwenye—kwenye mchanga, wakati mwanamke fulani alikuwa ameshikwa katika uzinzi. Kamwe Yeye hakuandika hata neno moja. Kwa nini? Alikuwa Ndiye lile Neno. Unaona? Alikuwa Ndiye Neno. Haikumbidi kuliandika; maisha Yake yaliliishi Hilo. Yeye alikuwa Neno. Kama Yeye . . . "Nisipozifanya kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi." Mnaona? "Kama sifanyi vile hasa Neno lilivyosema ningefanya, basi Mimi si Neno. Lakini kama . . . " Hivyo ndivyo alivyomaanisha. Yeye ni Neno.

36 Kwa hiyo sasa jitayarisheni sasa kwa ajili ya—kwa ajili ya mkutano ujao wa uponyaji na ushirika. Tungefurahi mkiwa pamoja nasi mkiweza. Kama hamwezi, itatubidi kufumukana mara moja.

37 Na msisahau, niombeeni na mumwombee mke wangu, mwanamke kipenzi kuliko wote katika ulimwengu mzima, na—na kwa watoto wangu. Na sasa nimewadai, kila mmoja, kwa ajili ya Bwana Yesu.

38 Sasa, Becky ni rika la "ricketta" mdogo, mwajua, na ni "tineja" m—mdogo tu, kama tulivyokuwa tukiwaita. Halafu basi, yeye yuko tu kwenye umri huo. Lakini, sasa, yeye ni msichana mzuri sana, nami nina—ninamshukuru Bwana kwa ajili ya jambo hilo; havuti sigara, hanywi pombe, hazururi kwenda huku

na huko, hafanyi lo lote. Lakini yeye yuko tu kwenye umri huo, yeye—yeye hajali. Hataki kwenda kanisani, na, kama akienda, yeye anaketi kule nyuma na kutafuna peremende, anaamka na kutoka nje. Hiyo, unaona. Ninataka kumwona amejazwa na Roho Mtakatifu.

39 Ninataka kumwona Joseph, ninamtaka mvulana huyo. . . Ninaamini ya kwamba siku moja wakati siwezi kutembea kwenda mimbarani tena, ninataka kuchukua Biblia hii ya zamani iliyochakaa na kumpa yeye, niseme, "Joseph, dumu Nayo, mwanangu." Ndipo niko tayari kupanda kwenda juu. Ninataka kusikia upepo ukivuma mahali fulani, niangalie juu, nipunge mkono wangu, niende zangu.

Na tuombe.

40 Baba Mungu, maisha yetu yote yamefungamana na Hilo, kwa sababu ni Wewe na Wewe Ndiwe Maisha yetu. Sasa kuna wengine hapa, Bwana, ambao—ambao hata wanashikilia hii Ishara niliyonena habari zake. Wao wamepata hiyo Ishara, na hata hivyo wao ni wagonjwa. Nami ninataka kuzungumza usiku wa leo juu ya kuwatia moyo, ku—kuwatia moyo kuchukua hizo haki walizopewa na Mungu. Wana haki ya kumshida huyo ibilisi. Yeye ameshindwa tayari, naye anawadanganya tu. Ninawadai, Baba.

41 Sasa, nisaidie kunena Neno. Nena kupitia kwangu, Bwana, pamoja na mihtasari hii midogo niliyoandika hapa, na Maandiko machache yaliyoandikwa. Ninaomba ya kwamba utanisaidia, Bwana, na uingie katika Neno na kuwapa imani kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Katika Jina la Yesu ninaomba. Amina.

42 Sasa upesi, ninawatakeni mfungue Biblia kwenye Kitabu cha Yeremia mlango wa 29, kama mkitaka kusoma. Ama, kama hamtasoma, liandikeni tu. Yeremia, mlango wa 29. Na tutaanzia kwenye kifungu cha 10 cha Yeremia, kifungu 10 cha mlango wa 29. Pia, tutasoma kutoka katika Luka, mlango wa 16, kuanzia kifungu cha 14.

43 Sasa, nitawapa somo langu, wakati—mnapo—mnapo—mnapofungua. Somo langu usiku wa leo ni *Kukata Tamaa*. Nami . . . Kukata Tamaa, na, sasa, mnajua kukata tamaa ni nini.

Na sasa tutasoma kutoka Yeremia mlango wa 29, kifungu cha 10.

> *Maana BWANA asema hivi, Babeli utakapotimiziwa miaka sabini, nitawajilia ninyi, na kulitimiza neno langu jema kwenu, kwa kuwarudisha mahali hapa.*
>
> *Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi,. . .* (Hilo si ni jambo zuri?). . . *asema BWANA*, wazo—*mawazo ya amani, wala si ya mabaya, kuwapa ninyi* kukubalika *siku zenu za mwisho.*

Nanyi mtaniita, nanyi mtakwenda na kuniomba, nami nitawasikiliza.

Nanyi mtanitafuta, na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote.

Nami nitaonekana kwenu, asema BWANA, nami nitawarudisha watu wenu waliofungwa, nami nitawakusanya ninyi, nikiwatoa katika mataifa..yote, na katika mahali pote, nilipowafukuza, asema BWANA;. . . *nitawaleta tena*, mpaka—mpaka *mahali* ambako *kutoka hapo naliwafanya mchukuliwe mateka*. Kurudi pentekoste!

Niliyaweka hayo, mimi mwenyewe. Haisemi hivyo. Hayo ndiyo niliyokuwa ninamaanisha kwa Kanisa.

Luka 16, tuanzie kifungu cha 15, ama kifungu cha 16.

Torati na manabii vilikuwa mpaka Yohana; tangu wakati huo habari njema ya ufalme wa Mungu hutangazwa, na kila mtu hujiingiza kwa nguvu.

"Kila mtu hujiingiza kwa nguvu." Si kutembea tu na kuingia ndani Yake, kwa urahisi, lakini hujiingiza ndani Yake kwa nguvu. Mnaona? Sasa, "Mnaponitafuta Mimi kwa moyo wenu wote, basi nitapatikana."

44 Naye aliahidi ya kwamba atarudi na kuwaleta watu, kutoka walikotawanyika kila mahali duniani, baada ya miaka hiyo sabini, kuwarudisha Yerusalemu walikotoka; Naye alifanya vivyo hivyo tu. Hiyo ni kweli.

45 Sasa tutazungumza juu—juu ya *Kukata Tamaa* kwa muda wa dakika chache sasa. Kwa kawaida hali ya dharura inahitajika ili kututia katika hali ya kukata tamaa. Mnaona? Ni jambo baya sana kwamba inabidi hilo litendeke hivyo. Lakini wanadamu ni goigoi sana katika nia zao, hivi kwamba inabidi kuwe na dharura. Jambo fulani linazuka, na wakati wanapofanya hivyo, basi lina—linawatupa katika hali hiyo ya kukata tamaa. Na kwa kweli, katika kufanya jambo hilo katika kukata tamaa, kunafunua kile wewe ulicho hasa. Inaonyesha wewe vile ulivyo hasa, katika wakati wa kukata tamaa. Kwa kawaida hutoa mambo yote mazuri yaliyo ndani yako.

46 Katika wakati wa kufa, nimewasikia watu walipojua ya kwamba walikuwa wanakufa, mambo waliyoweka siri maishani mwao mwote, wao, katika kukata tamaa walikuwa wanajaribu kuyakiri. Unaona? Na kujaribu, "Chukua jambo *hili* na ulisahihishe; nenda, tafadhali, nenda, lifanye," unaona, katika kukata tamaa. Walipaswa kuwa wamefanya jambo hilo hapo kabla, unaona, si kungojea mpaka wakati wa dharura. "Je! utanifanyia *kadha-na-kadha*?" Dharura husababisha kukata tamaa. Wakati, tunapaswa kufanya jambo hilo bila dharura.

47 Sasa tunaona, usiku wa leo, ya kwamba tunachukua mifano ya Pasaka. Na Pasaka ililiwa kwa dharura, katika nyakati za kukata tamaa. Unaona katika—katika Kutoka mlango wa 12, na kifungu cha 11 cha mlango wa 12, ninaamini ni hapo, inasema, "Kuleni pasaka hii mkiwa mmevaa viatu, mmejifunga mishipi viunoni, na fimbo mkononi mwenu," unaona, unaila katika kukata tamaa.

48 Wao walikuwa wameuona mkono mkuu wa Mungu. Walikuwa wameona miujiza Yake yote, na halafu walikuwa wamekuja chini ya ushahidi wa ile Ishara. Na wakati walipokuwa chini ya ushahidi wa ile Ishara, walikula ushirika katika—katika kukata tamaa, kwa kuwa walijua wakati huo Mungu alikuwa tayari kutoa hukumu.

49 Na ulikuwa ni wakati wa kutetemeka. Ulikuwa ni wakati ambapo kila mtu alikuwa anajichunguza mwenyewe, kwa sababu Neno la nabii halikuwa limeshindwa hata wakati mmoja. Lilikuwa limethibitishwa kwamba ni kweli. Lo lote alilosema, lilitukia vivyo hivyo kabisa vile alivyokuwa amesema. Nguzo ya Moto ilikuwa ingali pale. Na, halafu, nabii alikuwa ametangaza ya kwamba Mungu angepita juu yao tu wakati alipoona ile ishara mlangoni. Na ilikuwa ni kukata tamaa.

50 Ningewazia watoto walikuwa. . .wakati walipoona hayo mabawa mkubwa meusi yakishuka kutoka angani kama moshi ukitulia juu ya mji, vilio vikitoka katika kila nyumba, huenda ikawa watoto walienda kwa baba yao na kusema, "Baba, una hakika ya kwamba tuko chini ya hiyo ishara?"

Naye angeweza kwenda mlangoni, na kuangalia mwimo, kizingiti, aseme, "Mwanangu, hiyo ni kulingana na Neno Lake."

"Kumbuka, mimi ni mtoto wako wa kwanza. Baba, una hakika kabisa?"

51 "Mimi nina hakika! Hiyo ni kulingana na yale nabii aliyotwambia, naye ana Neno la Bwana. Alisema, 'Nitakapoona ile damu, nitapita juu yenu. Chukueni mwana kondoo mmoja kwa nyumba moja.' Nimewaingiza ninyi watoto wote ndani. Wewe ndiwe mtoto wangu mkubwa, lakini mtoto wangu wa kwanza. Hao ndio wanaokufa huko nje; lakini ile *pale* damu. Hiyo ndiyo iliyokuwa BWANA ASEMA HIVI. Kwa hiyo tulia, mwanangu, usifadhaike, kwa sababu Mungu ndiye aliyefanya ahadi hiyo. Unaona?"

"Vema, Baba, kwa nini umevaa viatu vyako? Kwa nini umeshika fimbo mkononi mwako? Kwa nini una kipande cha mkate katika mkono mmoja na mwana-kondoo katika mkono huo mwingine? Kwa nini mboga zenye uchungu na kadhalika? Mnazila kwa nini? Mbona unatokwa na jasho usoni?"

"Mwanangu, kifo kiko karibu kupiga." Unaona, ulikuwa ni wakati wa kukata tamaa.

52 Sasa, ninaamini ya kwamba tunaishi katika nyakati ambazo sisi tunaninii. . .Ama, vingine, siku tunazoishi zinapaswa kulifanya kanisa liingie kabisa katika kukata tamaa. Ninaamini, tangu ule ujumbe asubuhi ya leo uliotoka kwa Mungu, si kutoka kwangu, ninaamini unapaswa kulitupa kusanyiko hili lote katika kukata tamaa, kwamba tumecheza muda mrefu vya kutosha. Tumehudhuria kanisa muda mrefu vya kutosha. Hatuna budi kufanya jambo fulani!

53 Ni kwa nini kwamba tunaweza kuona ishara nyingine kubwa na maajabu yakifanyika juu ya wengine, na sisi je? Inapaswa kusababisha hali ya kukata tamaa, kwamba tumeyakinia, mbele za Mungu. Dalili za kuja Kwake zinapaswa kuleta kusanyiko hili zima, wakati tumelisoma katika Neno. . . .Na Roho Mtakatifu ametwambia, "Nendeni mahali fulani, jambo *fulani* litatukia," si kutuambia ilikuwa ni nini, lakini lingetukia. Tunaenda kule; linatukia namna hiyo. Magazeti ya kila siku yanaliandika, magazeti ya juma yanaonyesha picha yake. Tunarudi hapa na kuona hizo siri kuu, zilizofichwa katika Biblia, zikifunguliwa kwetu, katika mazingara mapya ambayo hatukujua hapo kabla, na inapatana kabisa na kule Kuja kwa Bwana Yesu.

54 Ndipo, mwisho wa hizo Jumbe, tunaona matendo ya Roho Mtakatifu mkuu, tunamwona akishuka na kuonekana dhahiri mbele za watu, hata akapigwa picha. Tunamwona akifanya kazi na kuonyesha ya kwamba si mwanadamu, si mhubiri tu, si kusanyiko fulani. Ni Roho Mtakatifu akionyesha jambo lile lile aliloonyesha wakati alipokuwa katika mwili wa Yesu Kristo. Sasa Yeye yuko ndani ya Mwili wa Bibi-arusi Wake. Inapaswa kututupa katika kukata tamaa.

55 Watu hao walikuwa wameuona mkono wa Mungu. Na usiku ule wa ushirika, waliula kwa. . .katika kukata tamaa, kwa sababu walijua ya kwamba jambo fulani lilikuwa karibu na kutukia. Nasi tunajua jambo fulani liko karibu kutukia. Basi kumbukeni, kule Kuja kwa Bwana kutakuwa ni kuondoka kwa ghafla na kwa siri. Yeye atakuja na kumchukua kama mwizi usiku. Na kuwazia ya kwamba kama mtu fulani, mara, kuna watu wa familia yetu ambao wameondoka, nawe umeachwa! Hilo linapaswa kututupa katika kukata tamaa, ya kwamba, kwa neema ya Mungu, hatutaachwa nyuma. "Kama kuna jambo lo lote sitaki . . . Usininii, usiniache, Bwana."

56 Siku chache zilizopita nilikuwa nikimsikia Mel Johnson akiimba ule wimbo:

> Nikumbuke wakati machozi yanadondoka,
> naam,
> Nikumbuke wakati marafiki hawako karibu;
> Na nitakapovuka mto huu wa Yordani,
> Utakapokuwa unaita majina, nikumbuke.

57 Na katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, ninataka jina langu liandikwe. Ninataka Yeye anikumbuke majina yaitwapo. Nalo linanitupa katika kukata tamaa, yaani, kama Paulo alivyosema, "Baada ya mimi kuihubiri Injili nitakuwa m—mwizi wa kujificha melini, nitakuwa wa ku—kukataliwa?" Linaweza kutukia. Kwa hiyo linanitupa katika hali ya kukata tamaa, kukata tamaa, kuwazia, baada ya miaka hii yote ya kuhubiri, hivi ninge—ningeweza...ifikie mahali ambapo ningemkosea? Hatua ya pili ni nini halafu? Nifanye nini? Nalo linanitupa katika hali ya wasiwasi. Basi nifanye nini? Linanitupa milimani na mabondeni. Na ni vigumu, kwa sababu, wakati nikiwa pamoja na watu, sina budi kuwa mambo yote kwa watu wote, kusudi nipate kuwavuta wengine kwa Kristo, hata hivyo nikiwa na hiyo Ishara daima mbele yangu. Unaona?

58 Nami ninaona mambo yanayokuja, nawe huwezi kuwaambia watu. Unaona mambo mbalimbali, nawe unakatazwa. Hayo maono wanayonipigia simu, na wakati mwingine wangesikitika kama ungaliwaambia, nawe unajua vizuri zaidi kuliko kuwaambia. Na halafu, unaenda mbali mno katika maono mpaka kila kitu kinakuwa ni ono, nalo linakutupa katika hali ya wasiwasi. U—unaangalia na kusema, "Sasa je! niko katika ono?" Kama vile kuketi papa hapa, "Je! hili ni ono? Nimesimama wapi hasa?" Unaona, una—unajisumbua sana, unajipa kazi kubwa sana. Na unapata mambo kuwahusu watu ambayo unatamani usingejua. Watu ambao wanatamani mambo haya, kujua mambo haya, hawatambui huduma ya namna hiyo inachogharimu. Hamjui kinachoambatana nayo. Ndipo inakutupa katika kukata tamaa, "Bwana Mungu, ninajua nitawajibika."

59 Jack Moore aliniambia wakati mmoja, "Nisingependa kutakiwa kuwajibika kujibu kama itakavyokubidi kuwajibika, kwenye ile Siku ya Hukumu." Kasema, "Mungu amewaweka watu hawa mikononi mwako, nawe utatoa hesabu kwa ajili ya kila mmoja wao. Utawajibika kujibu kwa ajili ya huduma yako." Hayo yamekuwa kama miaka kumi na mitano iliyopita, ama labda kumi na minane. Na tangu wakati huo, nimekuwa katika kukata tamaa. Nifanye nini? "Jalia niseme tu yale usemayo, Bwana. Jalia niwaambie yaliyo Kweli ama nisiseme jambo lo lote. Linanitupa katika kukata tamaa."

60 Kisha ninapoona dalili hizi zikija, ninapoona Roho Mtakatifu akitupeleka kule, na kuileta Mihuri hii, na kuiweka namna hiyo. Kuzileta Nyakati za Kanisa na kuziweka mle ndani, kisha kushuka katika Nguzo kuu ya Moto kule nyuma, na—na kujifunua Mwenyewe. Kisha anashuka chini katika jambo hilo jingine, kwenye ile Mihuri Saba, na kuifunua. Na hata kuiweka katika magazeti ya kila siku na magazeti ya juma. Kisha anaingia na kuwachukua malaika wa Mungu, hao malaika saba wenye Jumbe saba, na kuthibitisha vile hasa Biblia ilivyosema. Kisha, kwenye wakati huo, anakuja na kuleta hiyo Mihuri...

hizo ishara, vimulimuli vya wakati wa mwisho, na kuvileta kwa watu na kuwaambia ni kitu gani, na yote kuhusu jambo hilo, na Bwana akitenda kazi pale pale akijionyesha Mwenyewe kwamba yuko. Halafu basi, moja kwa moja kama vile asubuhi ya leo, anakuja na kuhitaji ile Ishara kwa kila mtu. Ndipo ninyi ni watu wangu. Ninyi ndio niwapendao, hawa na hao wanaosikiliza kanda hizi, na kadhalika. Ndipo mnaona linaniweka kwenye kukata tamaa kwa namna gani.

61 Kukata tamaa. Ishara za kuja Kwake zinapaswa kumtupa kila mshiriki wa Kristo katika kukata tamaa sasa, juu ya nafsi zetu, juu ya hali ye—ye—yetu njema ya baadaye. Vema, tutakuwa nini kama tukiupata ulimwengu mzima? Sisi ni nini, tunaishi kwa ajili gani? Unafanya kazi kwa ajili gani? Unakula kwa ajili gani? Unafanya kazi sana kwa ajili gani? Upate kuishi. Unaishi kwa ajili gani? Upate kufa. Na hustahili kuishi mpaka uwe unastahili kufa. Ni kweli.

62 Nasi tunaona miujiza mingi sana ya kuponya, linapaswa kutuweka katika kukata tamaa.

63 Kama mvulana huyo mdogo. . .Je ninamwangalia Bibi Peckinpaugh sasa? Je! huyu ni Bibi Peckinpaugh? Je! wewe ndiwe uliyekuwa na yule mvulana hapa, huyo au mwingine? Mbona, huyo mwanamke yuko hapa ameketi papa hapa niliyekuwa ninazungumza juu yake. Ilitokea tu niliangalia pale na kumwona.

64 Sasa, kama Mungu anaweza kufanya jambo hilo kwa mvulana huyo mdogo, inapaswa kuwatupa katika kukata tamaa.

65 Mtu fulani kutoka huko New Albany, huenda akawa hapa usiku wa leo. Yeye ni rafiki wa Ndugu yangu Roberson. Alikuwa na mvulana mdogo hapa. Nafikiri mkewe alikuwa na kansa wakati mmoja na akaponywa. Na—na sasa, mvulana huyo mdogo ana pumu zimemshika vibaya sana mpaka ako katika hali mbaya sana. Jamaa mdogo, kansa karibu imejaa kooni, yeye mwenyewe. Mnaona? Halafu basi akamleta mvulana huyo mdogo, naam, naona mkono wake umeinuliwa huko nyuma, kule nyuma, aliombewa asubuhi ya leo, mnaona.

66 Kukata tamaa! Wakati mkewe alikuwa karibu ya kufa kwa kansa, alijua ya kwamba Mungu angeweza kumponya. Na kama Mungu angeweza kumponya mkewe, Mungu anaweza kumponya mvulana huyo. Na inamtupa katika hali ya kukata tamaa. Unaona? Huna budi kuja; na wakati umekata tamaa, ndipo Mungu atakusikia. Lakini kama wewe ni goigoi tu, hujali anakusikia ama hakusikii, vema, basi hicho ni kitu kingine. Unasema unajali, lakini inahitaji kukata tamaa upate kufanya jambo hilo.

67 Ninaamini ya kwamba sababu ya sisi kutokuwa na kukata tamaa ni kwa sababu ya kukosa upendo, Mungu, upendo wa

Mungu. Ninafikiri kwamba upendo wa Mungu husababisha kukata tamaa. Kama Mungu yuko ndani yako, ile Ishara imo ndani yako, nawe unaona hali za nyakati hizi, na watu wakigaagaa dhambini jinsi wanavyogaagaa, itakutupa katika kukata tamaa. Ninaamini itakutupa.

68 Sasa, Neno linasema dhahiri, kama ukitaka kuliandika jambo hili, katika Wagalatia 5:6, ya kwamba, "Imani hutenda kazi kwa upendo." Mnaona? "Imani hutenda kazi kwa upendo." Na njia pekee ambapo wewe unaweza kuwa na imani, ni kuwa na upendo kwanza. Kwa sababu, hata hivyo, imani ni kichocheo cha upendo. Kishawishi, hivyo ndivyo hasa ninii i—imani ilivyo. Ni kichocheo cha upendo. Sasa, wewe, kama huna upendo, huwezi kuwa na imani. Unaona?

69 Unawezaje kuwa na imani kwa mke wako kama humpendi? Hiyo ni katika *fileo*. Sasa, ni vipi kwa wa *agape*, kwa Mungu? Inawezekanaje kama humpendi Mungu?

Kama ulisema ulimpenda mke wako, na usimwambie juu ya jambo hilo, na msiketi hata kidogo na kufanya mapenzi naye, kumwambia unampenda, kumbusu, kumkumbatia, na kumwambia ndiye mpishi aliye bora sana nchini, mambo yote unayojua, na jinsi anavyopendeza, na jinsi unavyompenda; usipofanya jambo hilo, yeye hatajua hilo kamwe. Njia ndiyo hiyo. Kama unampenda, mwonyeshe.

70 Hivyo ndivyo tunavyofanya kwa Mungu. Tunapompenda, tunamwambia kuhusu jambo hilo. Tunaketi chini na kumwabudu, na kusujudu. Na, unaona, upendo unatuelekeza kwenye jambo hilo.

71 Sasa, vipi kama jambo fulani linapaswa kufanywa kwa mke wako? Mbona, lingekutupa katika kukata tamaa kulifanya. Vipi kama mtu fulani akisema ya kwamba mke wako ana kansa? Vipi kama mtu fulani akisema mke wa—wako ana TB, naye yuko karibu kufa? Hata hivyo, wewe uta—utafanya jambo lo lote. Unaona, litakutupa katika kukata tamaa.

72 Na hilo ni jambo kama hilo vile vile. Hatuna budi kuwa na upendo kabla hatujakuwa na imani. Nayo imani. . . Tunapokuwa na upendo halisi, unafanya nini? Unaisukuma imani yetu nje huko vitani kwa ajili ya Mungu. Unaona? Upendo halisi wa kiungu kwa Mungu na kwa Neno Lake na kwa watu Wake, utaisukuma imani huko nje. Upendo unashika tu imani, na kuninii tu, "Hima, twende!" Na hiyoo inatoka, maana hivyo ndivyo upendo unavyofanya.

73 Yohana 14:23, Yesu alisema, "Mtu akinipenda Mimi, atayashika Maneno Yangu." Sasa huwezi kuyashika maneno Yake bila kuwa na imani katika yale aliyosema. Kwa hiyo, unaona, kama mtu anampenda Mungu, basi yeye hushika Neno la Mungu. Kama alisema, "Mimi ni Bwana aliyekuponya," yeye anaamini hilo. Upendo unamfanya aliamini, kwa sababu upendo

unatawala yote. "Nijaponena kwa lugha za mwanadamu na za Malaika, nisiwe na upendo, si kitu mimi, unaona. Nijapokuwa na imani kuihamisha milima, wala sina upendo, si kitu mimi." Upendo hutawala mambo yote, kwa sababu Mungu ni upendo, Mungu wa upendo. Sasa, naam, bwana! Kama Yesu alisema, "Mtu akinipenda Mimi, atayashika maneno Yangu."

74 Tunajua ni kweli ya kwamba Mungu atakutana na mtu anayekaribia kukata tamaa. Sasa, sote tunajua jambo hilo. Lakini kwa kawaida inahitaji jambo fulani kutuingiza hapo, kwenye huko kufa moyo, kukata tamaa. Inahitaji jambo fulani kufanya hivyo.

75 Tunaona, katika Yakobo 5:15, ya kwamba Biblia ilisema hivyo. "Ya bidii na yenye nguvu," hiyo ni kukata tamaa, "kuomba kwa bidii na nguvu kwa mtu mwenye haki kunafaa sana. Wakati mtu mwenye haki, mzuri, anapoingia kwenye utungu," ama uchungu kwa nafsi, ama utungu, moja ya hayo. Na—nafikiri uchungu ndilo neno bora zaidi. Utungu, ama uchungu, ama lo lote unalotaka kuliita. Lakini wakati na—na—nafsi inapoingia katika—katika hali ya kukata tamaa, katika utungu, maombi yanayofaa na ya bidii ya mtu ambaye anaweza kuonyesha ile Ishara, yanafanya jambo fulani. Unaona?

76 Angalia vile Biblia ilivyosema hapa pia, katika Yakobo 16, 5:16, ilisema, kama . . . "Tukiungama dhambi zetu," kujiweka sawa, kujiweka tayari kwa hilo, "kuungama dhambi zetu." Bila—bila dhambi . . . Wasihi watu wakuombee, tukiungama dhambi zetu sisi kwa sisi, na kuombeana. Hivyo ndivyo inavyotakiwa. Kwa upendo, upendo, kwamba nina imani ninaweza kuungama makosa yangu kwako; nawe unaweza kuungama makosa yako kwangu. Nami ninakupenda vya kutosha hata nitakuombea, nawe uniombee; nasi tutakaa na jambo hilo, kwa maombi yanayofaa na ya bidii, mpaka litakapojibiwa. Huko ni, huko ni kukata tamaa. Hilo ndilo tunalopaswa kuwa nalo daima wakati wote.

77 Hebu na tuchukue Maandiko machache kama mifano ya jambo hilo, ni jambo lililotukia, sasa, kwa dakika nyingine, kama kumi na tano, Bwana akipenda.

78 Yakobo, yeye alikuwa mtu, yeye kwanza alikuwa maskini ninii . . . kwa namna fulani mvulana asiyejali. Aliwazia akilini mwake mwenyewe ya kwamba alijua ya kwamba ile haki ya mzaliwa wa kwanza ilimaanisha kila kitu kwake, naye hakujali jinsi gani angeipata, bora tu aliipata. Na baada ya yeye kuipata, alidhania kila kitu kilikuwa shwari, kwa sababu alikuwa na haki ya mzaliwa wa kwanza. Alifikiri jambo hilo lilikuwa limetatuliwa. Alimjia ndugu yake wakati alipokuwa na njaa, akiingia kutoka kondeni, akitoka kuwachunga ng'ombe na kuwinda paa. Naye ndugu yake, ali—alihitaji nyungu kubwa ya chakula cha dengu, mbaazi mwitu na—na kadhalika pamoja. Huenda lilikuwa ni jambo la kujaribu mtu sana wakati mtu

ana njaa, baada ya kutembea mchana kutwa. Ndipo ndugu yake akasema, “Mimi ni karibu kuzimia. Nipe kidogo hiki.”

Ndipo akasema, “Vema. . .kama utaniapia nitapata haki ya mzaliwa wa kwanza.” Unaona? Hakujali jinsi alivyofanya jambo hilo, bora tu aipate. Naye alifikiri, wakati atakapoipata haki ya mzaliwa wa kwanza, hilo limetosha. [Ndugu Branham anapigapiga mimbarani mara nne—Mh.]

79 Pentekoste, hapo ndipo mlipokosea! Mlifikiri ati kwa sababu mlizaliwa kwa Roho, mlizaliwa kwa Roho wa Mungu, ile Haki ya mzaliwa wa kwanza, hilo lilitosha. Lakini huo ni mwanzo tu. Mnakumbuka katika ule ujumbe wa—wa *Msikieni Yeye*, jinsi ambavyo mtoto, baada ya kuzaliwa katika familia, anakuwa ni mwana. Alikuwa na haki ya haki ya mzaliwa wa kwanza, lakini ilibidi ajaribiwe, apate mafunzo ya mwana. Halafu kama hakuthibitisha kwamba ni mtoto mtiifu kwa mapenzi ya baba yake, basi hana budi, vema, hakupata ni—ninii. . .hakuwa ninii. . .hakufanywa mrithi. Hakurithi kitu, ingawa alikuwa ni mwana, lakini hakurithi kitu, kama hakuipenda kazi ya baba yake.

80 Na kwa hiyo wakati Roho Mtakatifu aliposhuka juu ya Wapentekoste nao wakaanza kuzirudisha zile karama na mambo yaliyokuwa katika kanisa; wao walidhani, ati kwa sababu walikuwa wamezaliwa kwa Roho, ya kwamba hilo lilitosha. Lakini, unaona, kulikuwa na kufanywa mwana mwenye mamlaka. Na baada ya mwana huyu kuthibitishwa kwamba ni mwana halisi, basi yeye alipelekwa mbele ya hadhara, na kuketishwa, na kubadilishwa mavazi, na kuketishwa pale juu; na ndipo kulikuwa na kufanywa mwana mwenye mamlaka, ya kwamba yeye alikuwa ni mrithi wa kila kitu alichokuwa nacho baba yake.

81 Mungu alifanya jambo lilo hilo kwa Mwanawe kwenye Mlima wa Kugeuzwa Sura. Yeye alitiwa uvuli na. . .ama wingu, na akageuzwa sura, na vazi Lake likawa jeupe kama jua, na sauti ikasema, “Huyu ni Mwanangu ninayependezwa Naye.” Musa pamoja na torati vimeshindwa. Na huyu ni Yeye, “Msikieni Yeye.” Aliwekwa mahali Pake. Mnaona?

82 Sasa Yakobo alifikiri, ati kwa sababu yeye alikuwa na haki ya mzaliwa wa kwanza ya kwamba kila kitu kililikuwa shwari.

Vivyo hivyo na Wapentekoste, nao wakaanza kuunda madhehebu, wa—wa umoja, wa utatu, na wa nafsi tatu, na kila namna ya madhehebu, na kuzozana na kuvutana wao kwa wao, ilithibitisha ya kwamba ile Ishara haikuwa inaonyesha. Uovu, wivu, ugomvi, mnaona, lakini hapo ndipo lilipofikia.

83 Sasa, unaona, Yakobo alifikiri jambo lile lile. Lakini katika hofu, usiku mmoja, na wa maisha yake, akashikwa na kukata tamaa, wakati alipofikiri ya kwamba, “Pale ng’ambo ya mto tu, ndugu yangu ananingojea aniue. Ataniua.” Unaona, ile haki ya

mzaliwa wa kwanza aliyokuwa amepata, ndicho kitu ambacho kingesababisha kifo chake.

Na wakati mwingine kitu hicho hicho unachopokea, kama Roho Mtakatifu, Ndicho, na umezaliwa mara ya pili kwa Roho, kama usipokuwa mwangalifu, kitu hicho hicho kitakuhukumu mwishoni. Hiyo ni kweli. Maji yale yale yaliyomwokoa Nuhu, yaliuhukumu ulimwengu. Kitu kile—kile ungekiita ushupavu wa dini huenda kikawa ndicho ambacho kinakuhukumu katika mwisho wa safari yako.

84 Sasa Yakobo alijua ya kwamba maisha yake yalikuwa karibu kwisha. Alifikiwa na mjumbe aliyekuja kumwambia ya kwamba ndugu yake, akiwa na watu mia nne wenye silaha, walikuwa wanakuja kukukutana naye, walijua alikuwa—alikuwa anakuja. Akashikwa na uoga. Akamtuma mtu amtangulie na maksai, na ng'ombe, na kondoo kutoa dhabihu ya amani kwa Esau. Ndipo, baada ya hayo, akatuma kundi lingine likiwa na mzigo mwingine wa bidhaa. Kisha akatuma kundi lingine likiwa na mzigo mwingine wa bidhaa, likijaribu kukutana naye kwanza, kujaribu kupoza hasira yake. Ndipo akaanza kufikiri, "Hilo halitamnyamazisha, kwa sababu labda yeye ni tajiri kuliko nilivyo mimi. Havihitaji." Ndipo akawachukua wake zake na watoto wake wadogo, na kuwatuma ng'ambo ya pili, ili kwamba Esau awaone hao watoto wadogo na wake zake. Na hakika wapwake wadogo wa kike na wa kiume, hangewaua. Halafu, yeye, angali bado, hakuliweza. Mungu anajua jinsi ya kumpata mtu. Yakobo akavuka kile kijito. Pale akapiga magoti.

Mwajua, yeye kwa namna fulani alikuwa namna fulani ya maskini dondoadume, kabla ya hapo. Samahani kwa tamshi hilo, lakini kwa namna fulani alikuwa maskini ninii . . . Alikuwa Yakobo. *Yakobo* maana yake ni "mdanganyifu," na hivyo ndivyo alivyokuwa. Lakini ilibidi jambo fulani litukie kwake. Pale katika kukata tamaa, pale wakati mauti ilipokuwa mbele yake . . .

85 Huenda kukawa na wanaume na wanawake wanaoketi hapa usiku wa leo, ambao, mauti iko moja kwa moja mbele yenu. Na njia pekee ambayo utaweza kupata kitu ambacho unataka, ni kuja kwa kukata tamaa. "Sina budi kulipata usiku wa leo. Ninalipata sasa, la sivyo nimekwisha. Kesho itakuwa ni kuchelewa sana. Sina budi kulipata sasa!"

Unapoomba ubatizo wa Roho Mtakatifu, ile Ishara, usiseme, "Vema, sasa nitaenda kule na kujaribu. Bwana, mimi, mimi nimechoka kidogo." Loo, rehema, usiamke kwenye kiti chako! Hata—hata usijaribu. Ukija, useme, "Nitapitia kwenye mstari wa maombi; Waweke mafuta kichwani mwangu, nitaona kama yatanifaa kitu," afadhali hata usiondoke ulipo. Mpaka utakapofika mahali hapo, mpaka kanisa lote litakapofikia mahali, ambapo ni kati ya mauti na uzima, huna budi kumpata

leo la sivyo uangamie, ndipo Mungu atakuja jukwaani. Inahitaji hali ya kukata tamaa kumleta Mungu jukwaani.

86 Yakobo alilia jinsi hajawahi kulia hapo kabla. Katika hali ya kukata tamaa alisihi mpaka akamshika Mungu. Na wakati alipomshika, alipigana miereka; si kwa dakika kumi na tano. Alipigana miereka Naye ili amwingize, nafsini mwake, usiku kucha; na hata hivyo alijua hakupata ile baraka, naye aliweza kushikilia mpaka baraka ikaja. Alipigana miereka katika hali ya kukata tamaa mpaka baraka ikaja. Ndipo, na wakati alipoona . . . mpaka Mungu alipokuja jukwaani. Na ndipo, katika hali ya kufa moyo, "Sitakuachilia uende," alipoanza kusikia baraka zikishuka juu yake.

Watu wengi husema, "Mungu atukuzwe, nimeipata sasa." Hapo umedanganyika. Naam! Mtu fulani anasema, "Loo, ninajisikia vizuri kweli kweli, Ndugu Branham, nilishuka nikaenda kule na kuomba. Loo, mitetemeko ikapitia juu yangu." Na huenda huyo alikuwa ni Mungu. "Niliona nuru kubwa mbele zangu." Huyo huenda bado alikuwa ni Mungu, lakini hilo silo ninalozungumza habari zake.

87 Biblia ilisema katika Webrania mlango wa 6, "Mvua huwanyea wenye haki na wasio haki," [Ndugu Branham anapigapiga mimbarani mara saba—Mh.] "vile vile tu." Sasa, hebu chukua ngano, kisha uchukue magugu, uyaweke kondeni. Na mvua kwa kweli ilitumwa kwa ajili ya ngano, lakini mvua inanyea magugu vile vile inavyonyea ngano. Na, mvua, na yale magugu yana furaha vile vile kwa mvua kama ngano vile vile, na ni mvua ile ile. Roho Mtakatifu yule yule anaweza kushuka juu ya asiyeamini na kumfanya atende vile vile hasa kama mwamini anavyotenda. Lakini kwa matunda yao wanajulikana; hilo ndilo ninalozungumzia; hiyo ndiyo ile Ishara. Naye Da- . . .

88 Na Yakobo, hasa, katika hali ya kukata tamaa, kasema, "Najua nimekuhisi, uko hapa pamoja nami, lakini sitakuachilia uende."

Mtu fulani analiona kwamba ni sawa, mwamsho mdogo wa kwanza, wanaamka na kuruka-ruka, na kukimbia kwenye marefu ya kanisa, wanasema, "Nimeipata, nimeipata, nimeipata." Loo, la. Aha. La.

Yakobo alikaa pale mpaka jambo fulani likatukia, ambalo lilimfanya atembee tofauti, likamfanya mtu tofauti, kwa sababu kwamba yeye alikaa mpaka jambo hilo likatukia. Naye aliweza . . . Biblia ilisema, "Alishikilia mpaka akashinda." Mtu anawezaje kumshinda Mungu? Lakini unaweza kumshinda. Unaweza kumshinda. Mwanadamu anaweza akamshinda Mungu.

89 Wakati mmoja kulikuwako na mtu jina lake Hezekia, alikuwa ameambiwa na nabii, "BWANA ASEMA HIVI, utakufa." Hezekia akaelekeza uso wake ukutani, na katika hali

ya kukata tamaa akalia, "Bwana, nihurumie. Nimetembea mbele Zako kwa moyo mkamilifu, nami ninahitaji miaka mingine kumi na mitano." Baada ya Mungu kumwambia ya kwamba jambo fulani litatukia; atakufa. Na, katika hali ya kukata tamaa, akabadilisha mpango wa Mungu. Hali ya kukata tamaa, hata hivyo, alilia kwa uchungu katika hali ya kukata tamaa.

90 Yakobo alikaa pale mpaka baraka ikaja, na kubadilisha jina lake kutoka "mdanganyifu" akawa "mtawala pamoja na Mungu." Hata taifa liliitwa kwa jina lake. Naam, bwana! Ni kitu gani? Matokeo yalikuwa ni kwa sababu aliingia katika hali ya kukata tamaa juu ya jambo hilo. Na kesho yake wakati alipokutana na Esau, hakuhitaji walinzi wo wote. Alitembea moja kwa moja akakutana naye. Unaona? Kwa nini? Yeye alikuwa ameingia katika hali ya kukata tamaa mpaka akapata hakikisho.

Nawe ingia katika hali ya kukata tamaa mpaka upate hakikisho. Usipoingia katika hali ya kukata tamaa, hata usije kuombewa. Hata usije kwenye madhabahu. Ngojea mpaka itakapokuwa ni kati ya uzima na mauti, kwako, ndipo jambo fulani litatukia. Kweli, kukata tamaa!

91 Ruthu aliingia katika hali ya kukata tamaa, wakati mmoja, wakati alipokuwa amesimama karibu na Naomi. Je! itambidi kurudi kwa watu wake, kwa wote aliowapenda, yote a—aliyoabudu, miungu yake na watu wake, ama angeambatana na Naomi? Afanyeje? Ndipo akaugua moyoni, kisha akalia, "Po pote uendako, nitaenda. Po pote utakapoishi, nitaishi. Utakapofia, nitafia. Utakakozikwa, nitazika. . . ama nitazikwa. Na Mungu wako atakuwa Mungu wangu." Haya basi, kukata tamaa! Mungu alimbariki, akampa mwana, Obedi. Obedi akamzaa Yese. Yese akamzaa, kupitia kwa Yese, akaja Yesu. Kwa sababu, kukata tamaa!

92 Kama maskini yule kahaba, Rahabu, alikuwa amekata tamaa. Alijua ya kwamba mauti ilikuwa mbele zake. Alikuwa chini ya hukumu. Naye akakata tamaa, kasema, "Nitawaficha ninyi wapelelezi. Nitafanya jambo lo lote. Ila tu, niapieni kwa Mungu wenu, na nyumba yangu itasimama." Haya basi.

Akasema, "Nitaninii. . . Kama utachukua ishara hii, itasimama."

93 Eliezeri alikata tamaa wakati alipopewa jukumu la kumtafutia Isaka bibi-arusi. Eliezeri wa Dameski alikuwa mtu mashuhuri. Alikuwa amependwa na Ibrahimu, naye alikuwa ameaminiwa na Ibrahimu aende akamtafute bibi-arusi, bibi-arusi anayefaa, kwa ajili ya mwanawe, Isaka. Kupitia kwake huyo angezaliwa Kristo.

94 Sasa, Eliezeri, akiwa ni mtu wa rohoni, alijua maana yake. Mke wa mtu huyo—huyo alipaswa kuwa ni mwanamke anayefaa. Naye atamchaguaje? Katika saa ya kukata kwake

tamaa, alipofikia ule mji, aliomba na kusema, “Bwana Mungu!” Jambo ndilo hilo. Unapokata tamaa, anza kuomba. “Bwana Mungu, jalia mwanamwali wa kwanza atakayekuja na kumpa maji ngamia na kunipa mimi maji, awe ndiye.” Aliomba katika saa ya hali ya kukata tamaa kwake.

95 Rebeka, yule mwanamwali wa kupendeza, akaja, akampa ngamia maji. Ndipo Eliezeri akasema, “Msinikawilishe katika safari yangu.” Ilimbidi kufikia wakati wa kuamua kama angeenda. Alikuwa ni mfano wa Bibi-arusi. Je! a—ataenda na akaolewe na mtu ambaye hajapata hata kumwona? Sasa, hilo ni jambo kuu. Hata hajapata kumwona, hata hivyo alikuwa amesikia tu kutoka kwa mtumishi wake.

96 Huyo ni mfano wa Bibi-arusi. Hamjapata kumwona Kristo. Lakini mnasikia, kwa watumishi Wake, jinsi Yeye alivyo. Mnauza kila kitu, mnaondoka makazi yenu, cho chote kile, kwenda kumtafuta Yeye. Sasa angalieni, naye akatoa uamuzi, mfano wa Bibi-arusi, akaacha makazi yake ya kimadhehebu, unaona, apate kwenda.

97 Yona, alitupwa baharini katika wakati wa tufani, chini ya kilindi cha bahari, katika tumbo la nyangumi. Matumaini yote ya kuokoka yalikuwa yamekwisha. Lakini ilitukia akakumbuka ya kwamba Sulemani, katika kule kuweka wakfu hekalu, alisema, “Bwana, kama watu wakipata shida mahali po pote na waligeukie hekalu hili na kuomba, basi sikia.” Huku akipinduka katika tumbo la nyangumi, alifaulu kupata mahali pa kupiga magoti, ninawazia, akiwa na matapiko ya nyangumi mwili mzima.

Hapo aliomba katika hali ya kukata tamaa. Na katika jambo hilo, kukata tamaa; yote aliyokuwa nayo katika tumbo la nyangumi ni mivuto michache tu ya oksijeni. Na katika mipumuo hiyo michache aliyokuwa anavuta, labda hakujua alikuwa anaelekea wapi, basi alisema, “Bwana, ninaamini ninaangalia juu kuelekea hekalu Lako.” Na huku amebakiza mipumuo michache tu, katika kukata tamaa, akaomba, katika hali hizo. Halijawahi kufanyika hapo nyuma, lakini alikuwa amekata tamaa. Akaomba, na Mungu akamhifadhi akiwa hai kwa siku tatu usiku na mchana, kisha akampeleka mahali pa kutolea ujumbe wake. Hali ya kukata tamaa!

98 Hana, mwanamke tasa katika Biblia, alikuwa anataka mwana, naye akaanza kufunga kwa ajili yake. Naye akafungu na kuomba mpaka hata yule kuhani pale hekaluni akafikiri alikuwa amelewa. Yeye alikuwa amekata tamaa kabisa! Huku wanawake wengine wakiangalia huyo mwingine alikuwa amevaa kofia ya namna gani; nanyi mnajua jinsi mambo hayo yalivyo; na huyo mwingine akiona kwamba walikuwa wamevaa nguo za namna gani, na kuzungumza juu ya mambo yaliyokuwa yanaendelea shambani. Lakini si Hana; yeye alipita moja kwa

moja katika umati huo wote akaenda madhabahuni. Alikuwa akifunga. Alitaka aibu yake iondolewe.

Ni tofauti gani leo. Karibu ni aibu kumpata mtoto. Wakati huo ilikuwa—ilikuwa ni aibu kutokuwa na mmoja.

Ndipo akapiga magoti. Wala hakujali cheo cha lile hekalu. Hakumjali mheshimiwa kuhani alipokuwa anatoka nje. Alikuwa katika huzuni kubwa sana hata manjonzi yalikuwa yakitiririka mashavuni mwake, naye alikuwa analia, katika kukata tamaa, "Ee Bwana Mungu, nipe mtoto wa kiune. Nipe mtoto wa kiune!"

99 Pia, angalia, yeye hakuwa mchoyo. Wakati Mungu alipomsikia, na akajibu maombi yake, na kumpa mwana, yeye alimrudishia Mungu mtoto huyo. Na kwa kuwa alikuwa tayari kutokuwa mchoyo baada ya Mungu kuyajibu maombi yake, Yeye alimpa nabii. Loo, hiyo ilikuwa ni baraka ya ziada. Loo, Yeye anavyo vingi, vitu hivyo vya ziada anavyotoa. Si mwana tu, lakini nabii. Wala hakukuwako na ono wazi kwa muda wa miaka mingi, mingi sana, katika Israeli. Samweli, nabii wa kwanza, kwa muda wa miaka mingi, mingi sana, kwa sababau mama fulani alikata tamaa; kwamba hangeweza kupata watoto, naye alikuwa amepita umri wa kuzaa, labda mwenye umri wa miaka sitini, sabini. Naye akaomba kwa kukata tamaa, hana budi kumpata mtoto huyu! Ilikuwa ni nini? Mungu alikuwa amenena naye, hapa na shaka.

100 Huwezi kukata tamaa mpaka Mungu anene nawe. Loo, Kanisa, amka na ujitikise! Finya dhamira yako, amka katika saa hii! Hatuna budi kukata tamaa ama tutaangamia! Kuna jambo linalokuja kutoka kwa Bwana! Ninajua jambo hilo kwamba ni BWANA ASEMA HIVI. Kuna jambo linalokuja, na ni afadhali tukate tamaa. Ni kati ya uzima na mauti. Litapita katikati yetu wala hatutaliona.

101 Kwa sababu yeye hakuwa mchoyo, alipewa nabii.

102 Yule mwanamke Mshunami alikuwa na mvulana mdogo ambaye nabii alikuwa amempa kwa Neno la Bwana, ingawa alikuwa mzee na mumewe alikuwa ni mzee. Hawakuwa na watoto, lakini alikuwa mwema kwa nabii hu—huyu. Naye alijua ya kwamba alikuwa mtu wa Mungu. Aliona ya kwamba alikuwa ni mtu wa heshima, mtu halisi. Akaja nyumbani, mumewe akiwa hayuko, na kadhalika. Alikuwa mtu mtakatifu. Waliweza kuona ya kwamba alikuwa mtu wa heshima. Alikuwa amemwangalia akifanya ishara na maajabu. Alimsikia akisema mambo ambayo yalitukia. Alikuwa mtu wa heshima, mtu mtakatifu.

Akamwambia mumewe, "Ninaona ya kwamba mtu huyu anayetutembelea ni mtu mtakatifu." Huyo mama wa nyumba hiyo, alijua ya kwamba huyo alikuwa ni mtu mtakatifu. Ndipo akamjengea nyumba ndogo kule kwa ajili yake, asije akaaibika. Angeweza kupitia kule kila alipotaka, na kadhalika. Akaweka ki—kitanda kidogo kule, na ninii—na dumu la maji,

na kadhalika, ili apate kuoga na apate maji ya kunywa. Na labda angemtuma mjakazi, ama mtu fulani, mnyweshaji, akiwa—akiwa na chakula cha kumlisha, akapitia pale na ku—kumwamkua, ama cho chote kile.

103 Na kwa hiyo wakati Eliya alipoona wema huu aliotendewa. Na imeandikwa, "Mnachowafanyia watoto Wangu, mnanifanyia Mimi." Kwa hiyo akaona jambo hilo, mwanamke huyo alikuwa anamheshimu Mungu hapo alipomheshimu nabii huyu, kwa kuwa aliishamwona Mungu katika nabii huyo. Na, kwa hiyo, yule mama hakutaka kitu cho chote kwake. Moyoni mwake yeye hakutaka kitu. Alifanya jambo hilo tu kwa sababu alimpenda Mungu. Hakutenda jambo hilo ili apate baraka yo yote. Alitenda tu.

104 Sasa, sasa Eliya alisema, "Nenda ukamwulize, je! nimwombee neno kwa mfalme? Mimi ni rafiki msiri wake. Au, kwa amiri jeshi, ni—ninamjua vizuri sana. Kuna fadhili fulani, jambo fulani ningaliweza kumtendea, ninataka kumpa kitu fulani kwa ajili ya vile alivyotufadhili. Ame—amenilisha. Amenipa vitanda vya kulalia. Na—na amekuwa mwema sana kwetu. Sasa nitende nini basi?"

Akasema, "La, mimi ninaishi tu kati ya watu wangu. Sisi—sisi tuna mali. Tuna vya kutosha, ni hayo tu. Hatuna haja ya kitu."

Ndipo Gehazi akamwambia, "Lakini hana watoto."

105 Mara Gehazi alipoona jambo hilo, hapana shaka nabii aliona ono, kwa kuwa alisema, "BWANA ASEMA HIVI, nenda ukamwambie katika wakati uliokusudiwa, ama wakati ufaao, mwaka mmoja tangu sasa, yeye atamshika mtoto mwanamume."

106 Basi mwana huyo akazaliwa. Alipokuwa na umri wa kama miaka kumi na miwili. . .Jinsi hao wazazi hapana shaka walimpenda sana mvulana huyu mdogo, mtoto wao wa pekee. Basi siku moja alikuwa huko shambani akikata ngano, akiwa na baba yake. Hapana budi ilikuwa ni mchana, alipata homa ya jua, nadhani, kwa maana alianza kulia, "Kichwa changu." Akazidiwa zaidi. Baba yake akamtoa shambani, na ikawa ni wakati wa dharura sana hapo, hata akamwita mtumishi wake, na kumtuma.

107 Mama yake akamshika pajani mwake mpaka adhuhuri, ndipo akafa. Angalia, mtoto wake wa pekee, ambaye alikuwa amepewa na Bwana, kwa maombi na ahadi ya nabii na BWANA ASEMA HIVI. Alijua kulikuwa na jambo fulani baya mahali fulani. Mambo hayakwenda ipasavyo. Mungu angewezaje kumpa mwana huyo kisha aache upendo wa—wake mama huyo uje kwa mtoto huyo mchanga? Hata hivyo hakuomba apewe huyo. Alikuwa ni mzee sana asingeweza kupata mtoto. Ilibidi mkono wa Bwana utamke jambo hilo. Mtu

fulani alilinena, nabii. Na hapo mtoto huyu katika hali hii, alikuwa amekufa, mwanawe wa pekee.

Kwa hiyo akamwambia mtumishi, "Nitandikie nyumbu, kisha umpande wewe, wala usipunguze mwendo. Kama mtu ye yote akijaribu kukusimamisha, usiseme neno, nawe uende moja kwa moja hata Mlima Kameli. Huko juu kwenye pango mahali fulani, huko nyuma, huko yuko mtumishi wa Mungu Aliye Juu Sana; yeye ambaye aliniambia, BWANA ASEMA HIVI, nitapata mtoto huyu. Ninataka kujua ni kwa nini Mungu amefanya jambo hili." Kwa hiyo akasema . . . "Ondoka uende moja kwa moja wala usimsimamishe huyo nyumbu. Mwendeshe mbio awezavyo. Mwendeshe mbio mpaka utakapofika kule." Kukata tamaa!

108 Ndipo nabii Eliya akasimama, akaangalia, na kusema, "Yule kule yule Mshunami anakuja, na, yeye, kuna jambo fulani mbaya kwake. Mungu amenilificha kwangu. Sijui kuna nini." Kasema, "Nenda ukamlaki. Nina . . . Hebu na tuharakishe. Kuna jambo baya."

Nabii akashikwa na hali ya kukata tamaa, mwanamke amekata tamaa. Unaona, walikuwa wanakutana; mmoja akitaka kujua Neno la Bwana lilikuwa ni nini, na huyo mwingine hakujua Neno la Bwana lilikuwa ni nini. Haya basi. Mmoja akitaka kujua, na huyo mwingine hakujua jambo hilo. Huyo mwanamke alitaka kujua, naye nabii hakujua. Kasema, "Mungu amenificha. Sijui la kumwambia atakapofika hapa."

Kwa hiyo alikuwa amekaribia kule basi. Akainua mkono wake, akasema, "Hujambo? Mume wako hajambo? Mtoto hajambo?"

109 Sasa, yule mwanamke alikuwa amefikia mwisho wa kukata tamaa kwake. Akasema, "Hawajambo!" Utukufu! "Hawajambo!" Kukata tamaa kwake kulikuwa kumwekwisha. Alikuwa amempata mtumishi wa Bwana. Kama hakuweko pale, angalikuwa bado yuko katika hali ya kukata tamaa. Lakini, unaona, yeye alikuwako. Akasema, "Hawajambo!"

Elisha akawazia, "Vema, ni jambo gani linaloendelea sasa?"

110 Kwa hiyo akakimbia na kuanguka miguuni pake. Hilo lilionekana kwa namna fulani jambo lisilo la kawaida, kwa hiyo Gehazi akamwinua tu. Kasema, "Mwache, usifanye hivyo." Eliya akamwambia mtumishi wake, "Usifanye hivyo. Mwache. Kuna shida fulani. Mungu ananificha." Ndipo huyo mwamanke akamfunulia ya kwamba yule kijana mdogo amekufa.

111 Sasa, nabii hakujua la kufanya. Akasema, "Gehazi, chukua fimbo hii ambayo nimetembelea." Alijua ya kwamba cho chote alichokigusa yeye kilibarikiwa, kwa sababu haikuwa ni yeye, ilikuwa ni Mungu ndani yake. Yeye alijua alikuwa ni nani. Alijua ya kwamba yeye alikuwa nabii. Kwa hiyo anachukua fimbo hii na kusema, "Gehazi, chukua hii, na uende ukaiweke juu ya mtoto yule. Na kama mtu ye yote akizungumza na wewe, ingia

katika hali ya kukata tamaa. Wala usimsalimu mtu ye yote, wala usiache ninii . . . Endelea tu mbele, usizungumze na mtu ye yote. Iweke hiyo juu ya mtoto huyo."

112 Lakini, yule mwanamke, hiyo haikumaliza kukata tamaa kwake. Hilo halikuridhisha kile alichojia. Akasema, "Kama Bwana Mungu aishivyo, si—sitakuacha mpaka utakapoenda na kumhudumia mtoto."

113 Ndipo Eliya akakata tamaa. Basi huyu hapa akaenda, barabarani, yeye na yule mwanamke. Na walipofika pale, ninii . . . watu wote walikuwa wametoka nje huko uani, wakipiga makele na kulia. Na yule mwanamke alikuwa amefanya jambo sahihi sana linaloweza kutendwa. Alimchukua yule kijana mdogo na akamlaza kwenye kitanda ambacho Eliya alikuwa amelalia. Hicho kilikuwa ni sawasawa tu na hiyo fimbo yake. Naye hakuamka pale, kwa hiyo kitu hicho hakingetenda kazi. Alitaka kujua jambo lingine.

114 Nabii akaingia ndani. Sasa, yeye yuko katika kukata tamaa. Sasa, atafanya nini? Nasi tunaona katika Biblia ya kwamba alienda huku na huko sakafuni, amekata tamaa. "Sijui jambo lingine la kufanya, Bwana. Mimi hapa. Uliniambia ninene lile kwa mwanamke yule, na BWANA ASEMA HIVI. Na ilikuwa ni vile vile kabisa nilivyomwambia, kwa sababu Wewe uliniambia. Sasa, huyo hapo katika shida, nami sijui la kufanya. Huyo hapo mvulana aliyekufa. Nifanye nini, Bwana?"

115 Hapana shaka Roho Mtakatifu alisema, "Kama Mungu yuko ndani yako, basi jilaze juu ya mtoto huyo mchanga." Muda si muda unajua, akasimama, akaenda mbio na akaweka mikono yake juu ya mikono yake, pua yake juu ya pua yake, kinywa chake juu ya kinywa chake. Na wakati alipojilaza juu yake, kijana yule mdogo akapiga chafya mara saba. Kukata tamaa kulikuwa kumekwisha.

Yule kijana mdogo akafufuka, kwa maana kukata tamaa kulimsukuma yule mwanamke mpaka kwa nabii, na kukata tamaa kukamsukuma nabii kwa mtoto mchanga. Na hali ya kukata tamaa katika wote wawili ikamleta Mungu jukwaani. Kukiwepo na upendo wa Mungu, na upendo kwa ajili ya watu wake, kulishusha upendo wa Mungu, na kukaitoa imani nje kwenye msatari wa mbele wa vita, ndipo kazi ikamalizika. Kesi ikaisha. Amina! Jambo ndilo hilo. Kukata tamaa kunasababisha jambo hilo. Bila shaka! Yeye hangeondoka.

116 Batimayo kipofu alifikiri Yesu atampita, akiwa ameketi kule nje langoni, kipofu mwombaji, kuomba sadaka. Muda si muda wajua, akasikia kelele; Yesu alikuwa anapita. Akasema, "Ni nani anayepita?" Mtu fulani akamsukuma akaanguka chini. Akasema, "Tafadhalini, jamani, ati ni nani anayepita hapa?"

Mmoja wao, vema, labda maskini mwanamke mfuasi mwema, akamwambia, akasema, "Bwana, hivi hujui ni nani huyo anayepita hapa?"

"La. Ninawasikia wengine wao wakisema, 'Kuna uwanja mzima wa makaburi uliojaa maiti kule juu. Kama wewe unawafufua wafu, nenda kawafufue.' Hivi huyo ni mkufuru ama mtu fulani?"

"La. Umewahi kusikia juu ya yule Nabii wa Galilaya, yule Nabii kijana Jina Lake anaitwa Yesu wa Nazareti?"

"La."

"Vema, unajua, katika Biblia inasema katika magombo yetu ya kwamba Mwana wa Daudi atainuliwa na kuketi juu yake. Ndiye Huyo."

"Ati Ndiye huyo? Ati huyo ni Yeye, anapita hapa!"

Kukata tamaa kukamsukuma kupiga makelele, "Ee, Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu!"

Usinipite, Mwokozi,
Unisikie;
Unapozuru wengine,
Usinipite.

"Ee, Yesu!"

Wengine wao walisema, "Nyamaza! Unapiga kelele sana."

117 Lakini alikuwa amekata tamaa. Kama akipita, huenda asipate nafasi nyingine. Huenda nasi tusipate pia; huenda huu ukawa ndio usiku wa mwisho. Kukata tamaa! Akapiga makelele, "Ee Yesu!" Haidhuru ni nani aliyemwambia anyamaze, yeye aliendelea tu kuita kwa sauti, kwa sauti kubwa zaidi. Walipomwambia anyamaze, hiyo ilimfanya apige makelele kwa nguvu zaidi. Alikuwa amekata tamaa. Hakuna mtu angaliweza kumnyamazisha. "Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu!" Naye akalia katika hali ya kukata tamaa.

118 Naye Mwana wa Mungu, akiwa na dhambi za ulimwengu juu ya mabega Yake, akienda Yerusalemu kutolewa dhabihu, wakati uo huo, kama dhabihu kwa ajili ya ulimwengu, alisimama njiani Mwake. Kukata tamaa, kilio cha kukata tamaa, kilimsimamisha Mwana wa Mungu. Kasema, "Wataka nikufanyie nini?" Loo!

Kasema, "Bwana, naomba nipate kuona."

Kasema, "Enenda zako, imani yako inakuokoa."

Hilo lilitosha. Kukata tamaa! Wakati kukata tamaa kunapokua tayari kupokea jambo fulani, mguso mdogo ulio hafifu kabisa kabisa, imani hulinyakua. Unaona? Yeye hakusema, "Sasa ngoja kidogo, ngoja kidogo, shikilia jambo hilo pale kwa muda kidogo, hebu nione kama ninaweza kuona sasa. Sijapata kuona mikono yangu, kwa miaka mingi. Hebu nione kama ninaweza kuiona. Sioni kitu bado." Wakati Yesu

aliposema, "Imani yako imekuokoa," hilo lilitosha. Hilo tu ndilo alilotaka.

119 Kukata tamaa kunataka kitu fulani, na wakati kitu hicho, haidhuru ni hafifu vipi, kinapokelewa, kinaaminiwa papo hapo, kwa sababu imani hushika wakati kukata tamaa kunapoisukuma. Unaona? Upendo mle ndani huchanganyikana nayo na kuileta kwake. Kukata tamaa kunafanya jambo hilo.

Kipofu Batimayo akashika ono upesi.

120 Petro, alikuwa ametaharuki sana, usiku mmoja baharini, wakati alipoingia katika kukata tamaa. Ndipo akaanza kupiga makelele, "Kuna kasoro fulani. Ninaona kivuli kikija, kinanijia kikitembea!" Chombo kilikuwa karibu kuzama. Akasema, "Kama ni Wewe, Bwana, niamuru nije Kwako juu ya maji." Ndipo akashuka chomboni na akaanza kwenda; ndipo akaogopa alipoanza kwenda, naye akaanza kuzama, na hali ya kukata tamaa . . . Ingawa ilikuwa ni kosa, katika kujaribu kufuata amri za Mungu, . . . Ninatumaini kanisa linapata jambo hilo. Mtu huyo alikuwa anafanya aliyoagizwa na Mungu kufanya.

121 Sasa, wewe Mkristo usiku wa leo, uko katika wajibu wako, ukijaribu kufuata uongozi wa Roho Mtakatifu; na kansa ikakushika ghafla, ama ma—mauti inakushika ghafla, kansa, kifua kikuu, cho chote kile. Ukiwa katika wajibu wako, una haki ile ile kama aliyokuwa nayo Petro.

"Bwana, niokoe, ama nitaangamia." Katika kukata tamaa yeye alipiga mayowe, ndipo mkono ukanyoshwa na kumwinua. Mna jambo lile lile. Lakini yeye alipiga mayowe, "Niokoe, Bwana!"

> Akasikia kilio changu cha kufa moyo,
> Kutoka majini akaniinua, sasa niko salama.
> Mnaona?

122 Hivyo ndivyo ilivyo, wakati unapopiga mayowe!

123 Labda mwanamke huyu, mama, cho chote kilichokuwa kwake, mwanawe mdogo, ama mjukuu wake, ama mpwake, ama ye yote yule, alipiga mayowe ya kukata moyo. Mungu akasikia.

124 Ndipo tunaona ya kwamba, katika kule kuzama, Mungu alimsikia. Akiwa kazini, alianza kuzama. Alishindwa. Haidhuru kama ukishindwa, hilo halina uhusiano wo wote na jambo hilo. Sote hushindwa. Sote ni wenye kushindwa, kwanza. Lakini tuna Mtu fulani anayesimama sasa mwenye mkono wenye nguvu, ambaye anaweza kutufikia na kutuinua juu ya maji.

125 Kama umekosea, mwanamke fulani amefanya kosa, mtu fulani amefanya kosa, mvulana fulani ama msichana amefanya kosa; usizame. Piga kelele, katika kufa moyo, "Bwana, niokoe, la sivyo nitaangamia!" Kata tamaa juu ya jambo hilo. Mungu atakusikia. Yeye daima husikia nafsi iliyokata tamaa. Hivyo ndivyo ninavyojaribu kuwaambia.

126 Bwana wetu mpendwa Yesu, Mwenyewe, katika uwanja wa vita ulio mkubwa kuliko vyote ulimwenguni, Gethsemane, alilia, katika kufa moyo. Je! azichukue dhambi za ulimwengu, ama abaki tu duniani pamoja na wanafunzi Wake wapendwa, jambo ambalo alitaka kufanya? Lakini angalia unyenyekevu Wake wakati Yeye akijinyenyekeza Mwenyewe, "Si mapenzi Yangu lakini Yako yatendeke," akajinyenyekeza Mwenyewe kwa Neno, Neno lililoahidiwa la Mungu wa Mbinguni.

Angalia, basi, akasonga mbele kidogo. Na kama alisonga mbele kidogo, ni zaidi sana vipi sisi tunavyopaswa kusonga mbele kidogo. Mnaona? Tena angalia, Maandiko yanasema hapa, katika Luka, ya kwamba Yeye aliomba kwa bidii. Ndugu, dada, kama ilimbidi Yesu kuomba kwa bidii, ni zaidi sana vipi sisi tunavyopaswa kuomba kwa bidii. Kama Kristo, Mungu wa Mbinguni, aliyefanyika mwili, ilimbidi kuomba kwa bidii, basi ni zaidi sana vipi sisi, wenye dhambi waliookolewa kwa neema, tunavyopaswa kuomba kwa bidii! Kama—kama uamumzi huo ulimtupa Mwana wa Mungu katika kukata tamaa, utafanya nini kwako na kwangu mimi? Hatuna budi kulia kwa kukata tamaa.

127 Mungu, katika siku hizi za mwisho, amejidhihirisha Mwenyewe namna hiyo kwetu, kwa ishara Zake kuu na nguvu, hilo linapaswa kutufanya tukate tamaa. Hiyo ni kweli. Na kupenda Kwake kutuponya sisi na kutuokoa, yapasa kututupa sisi sote katika kukata tamaa tupate kufikia kwenye lile Jiwe la uponyaji. Hiyo ni kweli.

128 Angalia, kama Florence Nightingale... Yule kitukuu wa marehemu Florence Nightingale aliyeanzisha Msalaba Mwekundu. Mmeiona picha yake katika kitabu, alikuwa na uzito wa ratili thelathini hivi. Kansa ilikuwa imemla. Huko London, Uingereza; walimleta kutoka Afrika, hadi London, Uingereza. Na akiwa kule katika kukata tamaa... Ndugu Bosworth alijibu barua yake na kumwambia, kasema, "Hatuwezi kuja Afrika."

129 Akajibu kwa barua, alimwambia nesi aandike na kusema, "Siwezi kusogezwa. Siwezi."

Akaonyesha ile picha. Mmeiona ile picha. Ni kwamba tu ilitubidi kuweka kipande kidogo juu yake. Ilikuwa tu imezungushiwa mshipi mdogo. Nilifikiri labda mtu fulani, nikiiweka kwenye kitabu, huenda angeitolea maneno kwa sababu alikuwa... mwili wake ulikuwa wazi sana pale, kwamba... ndipo tukaweka kitu kidogo cha kumfunika hapa. Alikuwa tu na kitambaa ki—kidogo, taulo imewekwa juu yake, juu ya nyonga zake. Lakini juu pale, hakukuwako na kitu. Na hata... Lakini tulifikiri tungeweka kipande kidogo cha karatasi juu yake na kupiga picha ninii... kuipiga picha. Kuwafanya watu wasio na msimamo mzuri wa kuwazia niani mwao, kwamba wasije wakanilaumu kwa kuichapisha picha hiyo kwenye gazeti.

130 Na halafu daktari aliposema ya kwamba hawezi kusogezwa, naye alijua ya kwamba nilikuwa ninaenda kuizuru Uingereza, huyo mwanamke akawaambia wamweke kwenye machela, na kumpeleka kwenye ndege, na kumleta London, Uingereza, na kumtuma mlinzi kule kwenye ndege kabla hatujashuka kwenda Buckingham Palace, wakamtuma mlinzi kule tuje tumwombee. Naye alikuwa amekwisha sana hata hakuweza kuzungumza nami. Iliwabidi kuinua mikono yake na kuiweka juu ya wangu.

131 Mnajua vile London ilivyo, baadhi yenu ninyi askari mmekuwa kule. Daima ni ukungu. Nami nikapiga magoti pale karibu na dirisha, naye . . .

Machozi yalikuwa yakitiririka. Alikuwa anataka kuninii . . . Hata sijui jinsi alivyopata unyevu wa kutosha kutoa machozi. Ni mifupa tu, yenye ngozi juu yake; na miguu ya—yake hapa juu kwenye nyonga haikuwa zaidi ya kama, ilionekana kwangu, kama inchi mbili hivi unene, ama inchi tatu. Mishipa yake ilikuwa imekunjamana. Vile alivyokuwa anaishi, sijui mimi. Mliona picha yake baadaye.

132 Nilipiga magoti kando ya kile kitanda. Sasa, alikuwa amekata tamaa; kama ningeweza kuja ama singekuja, walikuwa wamleta, hata iweje. Nami nikashuka nikaenda kule chini, moyo wangu ulikuwa unaugua ndani yangu, kwa imani ya maskini kiumbe hicho kidogo kilichokuwa kinakufa, nami nikaomba kwa moyo wote niliokuwa nao. Na wakati nilipoanza kuomba, njiwa mdogo akaja, akaruka dirishani, akaanza kutembea huku na huko, akiimba kwa upendo. Nilifikiri alikuwa ni wa kufugwa. Sikuwa nimekuwapo huko Uingereza ila kama kwa saa moja, nikiwa tu ninatoka kule kwenye uwanja wa ndege. Nami nilifikiri alikuwa ni wa kufugwa. Na wakati nilipoinuka, na kusema, "Amina," aliruka akaenda zake.

Ndipo nikaanza kuwauliza wale ndugu, kama wamemsikia yule hua. Nao walikuwa wakizungumza habari zake, na wakati nilipoanza kusema, "Je! mliona, huyo hua ana maana gani . . . ?" Ikatoka, "BWANA ASEMA HIVI, utaishi wala hutakufa."

Na anaishi leo. Kwa nini? Kukata tamaa. Kukata tamaa kulimsukuma mwanamke huyo kuchukua msimamo, aishi ama afe. Kukata tamaa kulipanga ya kwamba afike kule wakati ule ule niliofika mimi. Na ishara kutoka kwa Mungu, Yeye alituma njiwa, kutoa BWANA ASEMA HIVI. Kukata tamaa!

133 Wakati dada, maskini Hattie Waldorop wa Phoenix, Arizona, alikuwa anakuja njiani kando ya babara, katika mkutano wangu wa kwanza. Mwanafunzi msaidizi wa daktari pamoja na mumewe walikuwa wanamleta; kansa ya moyo. Yeye alikuwa amechukua msimamo wake, katika kujaribu kufika kule mkutanoni, lakini alikuwa ni mgonjwa sana alikuwa . . . hakuweza kupumua tena, damu ilikuwa ikirudi moyoni mwake mahali ambapo kansa ilikuwa imeula moyo wake. Sasa, kansa

ya moyo! Hiyo ni kama miaka kumi na minane, kumi na tisa iliyopita, labda ishirini, ilikuwa ni 1947.

134 Sasa, akamwambia mumewe na huyo daktari msaidizi, "Kama hata nikifia kwenye mstari huu, nipelekeni kule." Kukata tamaa. Alizirai. Sidhani alikuwa amekufa; anadai alikuwa amekufa. Sasa, huenda alikuwa amekufa. Huenda akasikia kanda hii, unaona. Sasa mimi—mimi—mimi . . . Yeye, yeye alidai alikuwa amekufa; sijui. Wao waliniambia, "Kuna mwanamke aliyekufa anayekuja mstarini." Basi huyo mwanamke alipokuja, alikuwa baridi. Na wakati walipomleta kule, Neno la Bwana likaja; ndipo nikaenda nikaweka mikono yangu juu yake, naye akaamka akaenda nyumbani akitembea. Hii imekuwa kama, ningesema, kwa usalama, miaka kumi na minane iliyopita, naye ni mwenye afya sana na mchangamfu . . . Atakuwa huko Tucson kunilaki nitakapofika kule. Kukata tamaa, "Hata nikifa nikiwa njiani, hata hivyo, lakini nipelekeni kule. Yeye aliwaponya wengine, ataniponya mimi." Kutaka!

135 Hebu mioyo yetu na ijazwe na upendo leo, na tuwe na bidii, na katika kukata tamaa. Baada ya kitambo kidogo, yaweza kuwa umechelewa sana.

136 Yairo wakati mmoja alikuwa na binti aliyekuwa anakufa. Yeye alikuwa ni mwamini wa mpakani. Alimwamini Yesu, lakini aliogopa kukiri jambo hilo, kwa sababu wangemfukuza kutoka katika sinagogi. Lakini daktari alikuja asubuhi moja, na kusema, "Yeye anakufa sasa." Kukata tamaa kukaingia. Yeye hakuthubutu, kwa ajili ya cheo chake, kuonekana akiwa pamoja na Yesu wa Nazareti, kwa maana angalipoteza nafasi yake kama kuhani.

Lakini nakwambia, wakati hali ya hatari ilipokuja, ilimtupa katika kukata tamaa. Ninaweza kumwona akitafuta koti lake dogo la mhubiri na kofia, na akaivaa. Huyu hapa anakuja kupitia kwenye umati wa watu, akisukumana; ambapo palikuwepo na mwanamke aliyekuwa ndiye tu wakati huo amegusa vazi lake, na kadhalika, nao wote walikuwa wanapiga makelele. Lakini akaingia na kusema, "Mwalimu, binti yangu mdogo amelala amekaribia kufa. Mwalimu, Mwalimu, msichana wangu mdogo amelala karibu ya kufa, na kama Wewe utakuja tu na kuweka mikono yako juu yake, ataishi." Loo, jamani! Kukata tamaa kunakufanya useme mambo wakati mwingine, kunakufanya ufanye mambo. Kunakufanya uingie kazini. Binti yake aliokolewa kwa kukata tamaa.

137 Hebu na tukate tamaa, kama maskini mwanamke yule aliyekuwa anatokwa na damu. Biblia ilisema alikuwa ametumia pesa zake zote, kwa madaktari, wala hawakuweza kumsaidia. Alikuwa ameanza wakati wa kuingia ugumba, kutokwa kwa wingi, na kutokwa na damu, wala haingekoma. Labda walikuwa wameuza shamba, nyumbu, farasi, na cho chote kile; wala hakuna kitu kingaliweza kumsaidia. Nao makuhani wao

walikuwa wamemwambia asikaribie kamwe kwenye kitu kama hicho. Lakini asubuhi moja aliangalia kule chini. Aliishi kule juu ukingoni, huko juu mahali lilipokuwemo lile shamba, naye akaona kundi kubwa la watu likikusanyika kumzunguka Mtu fulani kule chini, nao wakasema, "Ni kitu gani kile?"

Akasema, "Huyo ni Yesu wa Nazareti." Kukata tamaa kukaingia.

Akasema, "Mimi kwa namna fulani ni mdogo sana. Ni—ni-. . . Lakini kama tu ninaweza kugusa upindo wa nguo Yake, nitapata afya." Naye akampita kila kidomodomo na cho chote kile. Lakini basi akafikia mahali, akagusa vazi Lake, katika kukata tamaa.

Na alipoguswa, Yeye aligeuka na kusema, "Ni nani aliyenigusa?" Na wote wakakana. Lakini akaangalia pande zote. Alikuwa ana kipawa kikuu cha Mungu. Alikuwa Mungu; naye akampata maskini mwanamke huyo na kumwambia kutokwa kwake na damu kumeisha. Kukata tamaa kulimfanya afanye hivyo.

138 Kukata tamaa ndiko ku—kulikomsukuma malkia wa Kusini. Alisikia ya kwamba karama ya Mungu ilikuwa inafanya kazi ndani ya Sulemani. Kukata tamaa kulimsukuma kwenye hicho.

139 Kukata tamaa! Hao ni wanadamu, kama wewe, kama mimi. Hawakuwa tofauti na mimi na wewe. Walikuwa na zile hisi tano. Wanakula, na wanakunywa, na kadhalika, kama tunavyofanya na sisi, wanaishi na kufa. Walikuwa ni wanadamu.

140 Jambo hilo lilimtia katika kukata tamaa sana mpaka akachukua sehemu ya ufalme wake. Kulimsukuma kukamfikisha mahali hata hakufikiria juu ya Waishmaeli ambao wangemnyang'anya jangwani, siku zake tisini mgongoni mwa ngamia akivuka Jangwa la Sahara. Kukata tamaa! Anaenda, hata hivyo. Na wakati alipofika pale, hakuna jambo alilofichwa Sulemani ila aliyomwambia mambo yale aliyotaka kujua. Kukata tamaa! Yesu alisema, "Atasimama katika siku ya hukumu, pamoja na kizazi hiki, na kukihukumu, kwa sababu aliye mkuu kuliko Sulemani alikuwa hapa." Kukata tamaa!

141 Katika kufunga huenda nikasema jambo hili. Si muda mrefu uliopita, huko Meksiko, niliona kitu fulani kilichokata tamaa. Nilikuwa ndio tu nimeingia jukwaani, kwenye ule uwanja mkubwa wa michezo, na watu waliisha kuwa kule tangu saa 3 asubuhi hiyo, na ilikuwa inakaribia saa 4 kamili usiku huo. Mzee mmoja kipofu, usiku uliotangulia, kipofu kabisa kwa karibu miaka thelathini, alipata kuona, naye alikuwa anazunguka mjini siku hiyo, akishuhudia. Chungu nzima la nguo zilizochakaa, zimeweka labda katika lundo la yadi thelathini, arobaini, kubwa namna *hii*, ni shali zilizochakaa tu. Kulikuwako na labda watu elfu arobaini, elfu hamsini kule. Na kofia zilizochakaa na shali,

kwamba zilikuwa ni za akina nani, nafikiri ingewabidi kuamua jambo hilo miongoni mwao. Na mvua ilikuwa inanyesha sana.

142 Ndipo wakanishusha kwa kamba, juu ya ukuta fulani, na nikafika jukwaani. Mhudumu…Mtu anayeketi hapa, walimleta…Yeye na binti yake walitoka Michigan dakika chache zilizopita, wakazungumza juu ya Ndugu Arment. Tunamkumbuka hapa. Yeye yuko kwenye barabara za utukufu usiku wa leo. Ndugu Arment alikuwa pale, na akavua kabuti lake, na kusimama kwenye mvua, naye akampa Ndugu Jack Moore alivae, kwa sababu Jack alikuwa anatetemeka. Mwenyeji huyo wa Kusini alikuwa karibu kuganda katika mvua hiyo yenye baridi kule Meksiko. Naye alikuwa hapo amesimama pale.

143 Ndipo Billy Paul akanijia, mwanangu, na kusema, "Baba, itakubidi kufanya jambo fulani. Kuna mwanamke mdogo wa Kimeksiko kule chini amebeba maiti ya mtoto aliyekufa asubuni ya leo. Sina mabawabu wa kutosha kumwondoa mstarini." Kama kuweka mikono juu ya yule mwanamume kipofu kulimfanya aone, mtoto wake akiwekewa mikono atafufuka. Alikuwa Mkatoliki. Na, yeye, hawakuweza kumzuia.

Naye Ndugu Espinoza na hao wengine walikuwa wamemwambia ya kwamba, "Hatuna kadi nyingine za maombi. Itakubidi kungojea mpaka usiku mwingine."

144 Akasema, "Mtoto wangu amekufa. Alikuwa amekufa tangu asubuhi ya leo. Lazima nifike kule." Naye alikuwa anakuja, awe na kadi ya maombi ama asiwe nayo. Nao wakawapanga kama mabawabu mia tatu pale. Naye angepitia moja kwa moja chini ya miguu yao, na kuruka moja kwa moja juu ya migongo yao, na kukimbia na maiti ya mtoto huyu mchanga, na kuwaangukia. Haikuleta tofauti yo yote kwake; alikuwa anajaribu kufika mahali pale. Alikuwa amekata tamaa. Mungu aliisha nena na moyo wake, ya kwamba, "Mungu aliyeweza kufumbua macho, angeweza kufufua wafu." Loo, jamani! Yeye alikuwa amekata tamaa. Jambo fulani lilikuwa linawaka ndani yake.

145 Loo, enyi wagonjwa, kama mngeacha jambo hilo liwachome kwa dakika chache na mwangalie litakalotukia, kukata tamaa kwa namna hiyo. Mungu ambaye angeweza kumponya mvulana huyu mdogo usiku wa juzi, ambaye angaweza kumponya yule mama aliyekuwa na kansa, kumponya mtu huyu, na kufanya jambo hili, Bi Florence Nightingale, loo, makumi elfu! Yeye, ambaye, dhihirisho lisiloweza kukanushwa; kufufua wafu, na kuwaponya wagonjwa, na cho chote kile. Kama Yeye ni Mungu, anayeweza kufanya jambo hilo, Yeye ni Mungu jana, Yeye ni Mungu leo. Kata tamaa, ndipo utatendewa jambo fulani.

146 Ndipo, katika huko kukata tamaa, aliendelea kukimbia. Nikamwambia Ndugu Jack Moore, nikasema, "Yeye hanijui mimi. Hajapata kuniona. Hajui ni nani aliyepo hapa jukwaani. Maskini mwanamke huyo Mkatoliki, sasa, hakuweza kusema

hata neno moja la Kiingereza, kwa hiyo basi anajuaje kwamba ni nani?" Nikasema, "Shuka uende kule chini, na ukamwombee mtoto huyo mchanga, na hilo litamridhisha, naye ataenda zake." Nikasema, "Na hilo halitasababisha . . . " Kule chini ilikuwa ni mshindo tu wa makelele unaendelea. Yeye angeruka, na kila mtu angekuwa anapiga makelele. Angekimbia moja kwa moja juu ya mabega yao, na kuwaangukia papo hapo. Angesogea futi chache, halafu wangejaribu kumsukuma nyuma kabisa; naye huyu hapa angekuja moja kwa moja katikati ya miguu yao, huku amemshika mtoto huyu, akiwahangaisha mababwabu na cho chote kile. Halikuleta tofauti yo yote, yeye alikuwa anaenda kule. Ilimbidi kwenda kule! Haikuleta tofauti yo yote ilikuwa ni nini, ilikuwa ni lazima afike kule. Ilibidi mhudumu . . .

147 Sasa, hiyo si ni hadithi tu kama ya yule mwanamke Mshunami? Ila tu, haikuwa ni miaka elfu tatu mia tano iliyopita. Hiyo ilikuwa kama miaka mitatu iliyopita, ama minne. Unaona?

Wanaweza kuwa jambo lile lile usiku wa leo. Wakati kukata tamaa kule kule kunapotokea kutatupilia upendo na imani kule juu vitani, kudai yale unayotaka, kwa maana ni ahadi ya Mungu ya kwamba unaweza kuipata. Hiyo ni kweli kabisa.

148 Nikageuka; mimi, yule mhudumu, ama yule mwinjilisti mahali pale. Nikageuka. Nikamsikitikia mwanamke huyo, lakini hakukuwa na kukata tamaa. Unaona? Nikageuka na kuwazia, "Vema, Ndugu Jack atamwombea, na hilo—hilo linatosha." Nikageuka. Nikasema, "Kama nilivyokuwa nikisema sasa, imani . . . "

Nikaangalia kule nje, na kulikuweko na ono. Niliona mtoto mchanga ameketi kule, mtoto mdogo mweusi wa Kimeksiko hana meno. Alikuwa akinichekea, ameketi pale. Nikasema, "Ngoja kidogo. Ngoja kidogo." Kukata tamaa kwake kukamfanya Roho Mtakatifu abadilishe somo langu, akageuza macho yangu na kunionyesha mtoto wake ameketi pale. Hilo lilimrudisha Roho nyuma. Nikasema, "Ngoja kidogo. Ngoja kidogo. Nileteeni huyo mtoto."

Huyu hapa akaja na mtoto mdogo na blanketi ya bluu na nyeupe, yenye majimaji, iliyolowa maji, maiti mdogo mrefu *hivi*. Akaanguka, huku ameshika msalaba wenye sanamu mkononi mwake, ama rozari, kusema hizi "salamu Maria." Nikamwambia, "Ziondoe, si lazima."

Naye akakaribia mahali nilipokuwa, na akaanza kupiga makelele na mayowe, "Padre," maana yake, "Baba."

Nikasema, "Usiseme hivyo. Usiseme hivyo. Unaamini?" Naye akamwambia katika Kihispaniola, je! aliamini.

"Ndiyo," aliamini. Akamwuliza angeaminije. Akasema, "Kama Mungu anaweza kumpa yule mzee kuona, anaweza kumpa uhai mtoto wangu." Amina. Kukata tamaa kulimfanya afanye jambo hilo. Sikuhusika kamwe; niliona tu lile ono.

Nikasema, "Bwana Yesu, niliona ono la mtoto mchanga, huenda ikawa ni huyu."

Mnamo wakati huo akatupa miguu yake, akafanya, "Wha! Wha! Wha!"

Nikasema, "Mfuate mpaka kwa daktari. Pata taari-. . . taarifa ya daktari ya maandishi, 'Mtoto huyo alikufa.'" Na daktari huyo akaandika hiyo taarifa, "Kupumua kwa mtoto huyo, moyo wake ulikoma asubuhi ya leo, ofisini mwangu saa tatu, akafa kwa nimonia maradufu." Loo, mtoto huyo mchanga anaishi huko Mexico usiku wa leo, nijuavyo mimi. Kwa nini? Kukata tamaa kuliingia katika moyo wa mama huyo, akimlilia mtoto wake, ambaye alikuwa amemwona Mungu akifanya. . . akiyapomnya macho ya kupofu, naye alijua Yeye angeweza kumfufua mtoto huyo aliyekufa.

149 Kukata tamaa! "Mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote, basi nitawasikia." Unaona?

150 Ule Ufalme! "Torati na manabii vilikuwapo mpaka Yohana. Tangu wakati huo, Ufalme wa Mbinguni umetangazwa, na watu hujiingiza kwa nguvu." Husimami tu na kusema, "Nishike kwenye ukosi, Bwana, unisukume ndani." Unajiingiza kwa nguvu. Unakata tamaa, kati ya Uzima na mauti.

151 Laiti ningalikuwa na wakati kwa ajili ya hadithi nyingine, niliyokuwa nikiiwazia sasa hivi, ya mwanamke fulani, msichana, aliyeendea njia mbaya, na jinsi alivyokuwa ameanza upya na kadhalika, mpaka nikasema, "Dada . . . "

Akasimama na kusema, "Ni—ninaamini nitakuwa sawa."

Nikasema, "La, la! Kaa hapo."

Na halafu, muda si muda wajua, akaanza kuomba kidogo, na mara akaanza kuomba kwa sauti kubwa na kubwa zaidi. Na baada ya kitambo kidogo akakata tamaa, akasema, "Ee, Mungu, uniokoe!"

152 Chama cha Walevi hakingeweza kuponya hilo. Hakuna kitu kingine kingaliweza. Lakini hayo macho makubwa, meusi yakaniangalia, na majonzi yakitiririka mashavuni mwake; akasema, "Jambo fulani limetukia." Loo, naam! Naam, bwana! Jambo fulani limetukia. Alikata tamaa.

153 Hebu na tuwe katika hali ya kukata tamaa juu ya jambo hili, ni kati ya mauti na Uzima.

154 Kama huwezi kukata tamaa, usipitie hapa. Kama umekata tamaa, njoo hapa na uangalie, u—utalipata mara ufikapo hapa.

155 Na tuombe. Katika kukata tamaa utafuteni Ufalme wa Mungu, utakuja juu yenu.

156 Baba yetu wa Mbinguni, ninakuomba katika Jina la Yesu, uturehemu, Bwana. Na uanzishe ndani yetu kukata tamaa. Ee Bwana Mungu, turehemu, ninakuomba, na jalia watu

wakutafute usiku wa leo kwa mioyo iliyokata tamaa. Tunajua uko hapa, Bwana. Ni wewe yeye yule jana, leo, na hata milele.

157 Na sasa, naomba watu hawa ambao wana ile Ishara, kwamba wamepita toka mautini wakaingia Uzimani, wamebadilika kutoka maisha ya zamani ya kilimwengu wakaingia katika mapya. Wamefanya hivyo. Damu imepakwa; na, Mungu, wape dalili ya Ishara. Naomba wachukue Ishara hiyo mikononi mwao, hao walio wagonjwa, waseme, "Mimi ni mzao ulionunuliwa wa Mungu. Niko ndani ya Kristo, na ndani Yake hamna magonjwa. Mimi niko ndani ya Kristo, na ndani Yake hamna dhambi. Mimi niko ndani ya Kristo, na ndani Yake hamna kutokuamini. Ninakataa kila kitu ambacho ibilisi ameniambia. Ninachukua Ishara yangu ya kwamba ninii yangu. . .'Alijeruhiwa kwa makosa yangu; alichubuliwa kwa maovu yangu; adhabu ya amani yangu ilikuwa juu Yake; na kwa kupigwa Kwake mimi niliponywa.' Na sasa ninashikilia ile Ishara, ya kwamba Mungu amenitambua, kusudi lile, Mtu, nimenunuliwa kwa Damu ya Bwana Yesu. Nami ninashikilia ile Ishara ya mauti Yake katika mikono yangu, kwa maana Yeye amefufuka tena, nami ni wake na Yeye ni wangu. Ninaenda na imani iliyo yakini, ya kwamba tangu usiku huu na kuendelea, ninamwamini Mungu, nami nitaponywa nitakapofika kule na kutimiza masharti."

Kwa sababu, maneno ya mwisho yaliyoanguka kutoka katika mdomo Wake, yalikuwa ni haya, "Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Tujalie, Bwana. Jalia kukata tamaa kuingie, kwa kuwa ninaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Naweza, taamini, ninaamini;
Naweza, taamini, ninaamini;
Naweza, taamini, ninaamini;
Yesu ameniponya sasa.

Loo, naweza, taamini, ninaamini;
Naweza, taamini, ninaamini;

(Wazieni tu, "Nimekusudia!")

Naweza, taamini, ninaamini;
Yesu ananiponya sasa.

158 Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] "Nimekusudia! Nimekusudia, kwa neema ya Mungu, ya kwamba sitakoma kamwe mpaka kwamba kitu Fulani kitakaponigusa mimi. Na ninapanda kwenda kule nikawekewe mikono."

Sasa, Mungu hajapata kutupungukia. Nami ninaamini Tabibu mkuu yuko karibu sasa. Ninamwamini Mungu aliyeliandika Neno, ninamwamini Mungu aliyetoa dhabihu; ninaamini Ishara ya Mungu ambayo hutuosha na dhambi usiku wa leo, ile Ishara, Uhai Wake Mwenyewe, uko hapa pamoja nasi. "Nitakuwa pamoja nanyi, hadi ukamilifu wa dahari. Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, hata hivyo ninyi mtaniona, kwa maana nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu,

hata ukamilifu wa dahari." Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Ninamtumainia Yeye. Ninaamini ya kwamba Yeye atafanya jambo hilo. Nawe je? ["Amina."]

159 Sasa, mara tu ninapoanza jambo hilo, ninaona maono yakitokea, amina, maono makubwa ya Bwana, akinena mambo makuu. Amina! Nikianza jambo hilo, tutakuwa hapa usiku kucha. Mtaamini jambo hilo? Mnaamini? Amina! Ninaamini jambo hilo kwa moyo wangu wote.

160 Maskini yule mama anayeketi pale kutoka kwa Ndugu Palmer, simjui. Ametoka Georgia, naye ana shida ya kike. Kama ataamini ya kwamba Mungu atamponya, Yeye atamponya. Sijapata kumwona mwanamke huyo maishani mwangu, lakini hiyo ndiyo shida yake.

161 Maskini mwanamke huyo, sijui kama amewahi kusikia juu ya Ujumbe huu, ama hajasikia, lakini wakati nilipokuwa nikihubiri hapa, nilimwona. Amini tu jambo hilo na uone kama hiyo ni kweli. Amina. Kama utaamini tu! Hiyo ni kweli.

162 Mama yule anayeketi papa hapa nyuma akiumwa na mgongo, anaumwa sana, jina lake ni Bibi Wisdom. Kama utaamini kwa moyo wako wote, Yesu Kristo atakuponya. Sijapata kumwona mwanamke huyo maishani mwangu, lakini anaketi pale, anaumwa. Amevaa gauni la majanao. Hiyo ni kweli? Vema. Hatufahamiani? Naam. Vema, bwana. Enenda nyumbani, uwe mzima. Yesu Kristo anakuponya. Amina.

163 Mwanamke mwingine aliyeshika jambo hilo sasa hivi, shida ya mgongo, ameketi hapa. Ana shida ya mgongo. Ana mvulana fulani, naye anaumwa na kichwa. A-ha. Hiyo ni kweli. Jina lake ni Bi. Parker. Aminini kwa moyo wako wote, na Yesu Kristo atawaponya ninyi wawili. Amina! Sisi hatufahamiani. Hiyo ni kweli kabisa. Amina! Amini kwa moyo wako wote.

164 Hapa pana mzee ameketi hapa nyuma kutoka Michigan. Ana shida ndani ya maskio yake. Loo, anafikiria sauti, shida ya kiroho. Hiyo ni kweli? Unaamini ya kwamba—ya kwamba . . . Hujui kama ni Mungu, ama ni kitu gani kinasema nawe. Unasikia makelele masikioni mwako. Mimi hunijui kabisa. Kama hiyo ni kweli, inua mikono yako, na hayo ndiyo yanayotendeka. Hazitakusumbua tena, Yesu Kristo anakuponya.

Mnamwamini yule Tabibu mkuu? [Kusanyiko linashangilia, linasema, "Amina."]

165 Ningetaka kuzungumza nawe, lakini, kutoka Norway, nawe hufahamu; lugha yako ni ya Kinoruwei. A-ha. Vema, mwambie aende nyumbani, akiamini, dada, kama unajua kuizungumza. Mwambie kuumwa kwake na kichwa kutamwacha. Sasa, mnajua simjui. Amekuja hapa kutoka Norway, apate kuombewa. Rudi, ukiwa mtu mwenye afya. Amina.

166 Loo! "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele!" Ni kitu gani? Ni ile Nguzo ya Moto. Ni Roho Mtakatifu. Ni ile Ishara, ya kwamba Yesu Kristo anaishi. Na wakati watu, zamani za kale, walipomwona akifanya mambo hayo, Yeye alijua wazo lao, kwa maana Yeye ni Neno. "Nalo Neno ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, na huyatambua mawazo na makusudi ya moyo." Amina.

167 Niliona maji yakimulika, na kijana huyu akija. Yeye alisikia, na akasoma kitabu kule, na kilichoandikwa, katika Kinoruwei. Akaanza kufahamu; mtu fulani akazungumza naye. Yeye ana shida, lakini, kama ataamini kwa moyo wake wote, Bwana Yesu atamponya. Ametoka mbali, na ni mtoto maskini, kwa hiyo, akijaribu kujiingiza kwa nguvu. Nasi tutaweka mikono juu yake, hivi punde.

168 Je! mnaamini? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Amina! Ni ajabu vipi! Loo, jamani! "Tabibu mkuu sasa yu karibu!" Dada, Yuko wapi yule Dada Ungren, na yule dada mwingine kwenye piano? Ninawatakeni mje upesi sana, tafadhali, mtupe wimbo, "Yule Tabibu mkuu yuko karibu sasa, Yesu mwenye huruma."

169 Ninawataka watu walio kwenye marefu haya ya kanisa *hapa*, wanaotaka kuombewa, naomba washuke waje upande huu *hapa*, marefu ya upande mmoja tu ya kanisa kwa zamu. Ndugu Neville, fanya hivyo tafadhali. Yuko wapi Ndugu Capps ama mmoja wa hao viongozi wa nyimbo? Vipi kuhusu Ndugu Ungren, ama Ndugu Capps, ama mtu fulani, aje hapa, ataimba, tafadhali oangoze wimbo huu kwa ajili yetu. Je! Ndugu nanii . . . Yuko wapi mmoja wa hao ndugu? Vema, Vema, bwana, hilo ni zuri. Vema. Kila mtu katika maombi!

170 Kumbukeni, kukata tamaa! Unaona kile kukata tamaa kutakavyofanya? Kukata tamaa kutakuvusha bahari. Kukata tamaa kutakusukuma utoke katika jimbo lingine. Kukata tamaa kutakupeleka mahali po pote. Baba mzee wa thamani na bintiye, waliokata tamaa, walijaribu kuingia, kuingia humu, kwa hali zote, na wakaketi hata hivyo; muda mfupi uliopita Roho Mtakatifu akaleta jambo hilo hapa mkutanoni, kabla tu sijafika hapa. Loo!

> Pweke limetukuka,
> Jina Lake Yesu.
>
> Ni Tabibu wa karibu,
> Tabibu wa . . .

Bwana Yesu, tujalie, yasikie maombi ya mtumishi Wako, Bwana. Ninaomba ya kwamba utakutana na kila mmoja wa hawa tunaoombea, katika Jina la Yesu.

> . . . . dawa yake njema
>
> Imbeni malaika,
> Sifa za Yesu Bwana;
> Loo, pweke limetukuka,

Hebu wale waliokata tamaa sasa, ambao mnajua kweli mtaponywa . . . Wazieni tu, nijuavyo mimi, asilimia mia moja waliponywa, kutoka Jumapili iliyopita usiku, waliponywa juma hili.

Tabibu wa ajabu . . .

171 Angalia, Yeye anakuja. Mnaona, Tayari amewaponya. Analeta Neno Lake, analithibitisha, anaonyesha Uwepo Wake. Hakuna mtu anayeweza kufanya mambo hayo nje ya Mungu. Mnajua jambo hilo. Ni ishara ya Masihi. Nanyi mnajua mimi si Masihi, Kwa hiyo ni Yeye. Sasa, hapa Yeye amewathibitishia kila kitu.

Sasa, linapaswa kuwatupa katika kukata tamaa. Linapaswa kuchochea sana mahali hapa na kugusa ninii . . . La, inakuwa tu kama ki—ki—ki—kijiti cha kiberiti kwenye pipa la baruti. Bila shaka! Na linapaswa kuilipua imani, na—na upendo na kukata tamaa kuwasukuma watu hao na kuwaingiza moja kwa moja katika Ufalme wa Mungu, waamini kwa moyo wao wote. Je! mnaamini sasa, kila mmoja wenu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema. Sasa, Billy, wewe chukua . . .

172 Tony, niangalie hapa kwa muda kidogo. Sijakuona kwa muda mrefu sana, lakini wewe ni mgonjwa. Una ugonjwa wa kitu kama ugonjwa wa kuhara damu. Hiyo ni kweli. Utakwisha. Utakuacha. Niliona kitu hicho kikimfuata, alipokuwa akianza kuja pale. Hakuna kitu kinachoweza kufichwa Mungu sasa hivi. Sijapata kuona . . . Sijamwona Tony kwa miezi kadha, nadhani, lakini ninaona ana huo. Alikuwa nao; sasa hana.

173 Na tuinamishe vichwa vyetu. Hata jicho moja lisifunguliwe. Hata jicho moja lisiangalie. Hebu kila mtu awe katika maombi. Na Billy Paul ama Ndugu Neville, mmoja, ataita safu zinazofuata wakati unapofika. Sasa kila mtu na awe katika maombi. Tutajaribu sasa; marefu ya katikati yatakuja kwenye mkono wako wa kushoto mtakapoitwa, na vivyo hivyo ma—marefu ya mkono wa kushoto upande *huu* watakuja kwenye mkono wako wa kushoto hapo mtakapoitwa. Ndugu Neville atawaita.

Sasa, sijui kama kuna ye yote wa hawa ndugu hapa ambaye angetaka kusimama hapa na kuweka mikono yake juu ya watu hawa wanapopita hapa, pamoja nami? Ye yote wenu ndugu wahudumu, bila shaka mnakaribishwa kuja na kusimama pamoja nami kama ukitaka kufanya jambo hilo. Si jambo la kipekee. Mna haki ya kuwaombea wagonjwa vile vile kama mimi pia.

Ninajua Roho Mtakatifu yuko hapa. Mtu ye yote ambaye hangeamini jambo hilo, kuna kasoro kwao.

174 Vema, hebu na tuamini sasa kwa mioyo yetu yote, ya kwamba Mungu atatujalia mambo haya tunayoomba. Iweni na imani sasa. Msitilie shaka.

Na kila mtu na aombe, muombeane. Biblia ilisema nini? "Ungamanieni makosa yenu ninyi kwa ninyi; ombeaneni ninyi kwa ninyi . . ."

175 Nanyi watu mnaopitia mstarini, mara mikono hii ikiwagusa, nendeni moja kwa moja kutoka hapa mkiwa na furaha tu na kumsifu Mungu ya kwamba mmeponywa.

Vema, kila mtu katika maombi sasa wakati Ndugu Capps anapoongoza nyimbo.

Bwana Yesu, sasa tusaidie. Ninaomba, katika Jina la Yesu Kristo, ya kwamba Roho Mtakatifu atamgusa kila mtu, na naomba waponywe tunapozizingatia amri Zako za kuwawekea wagonjwa mikono. Ulisema, "Watapata afya." Tunaamini jambo hilo, Baba, katika Jina la Yesu. Amina.

Vema, kila mtu katika maombi sasa tunapoanza kuomba. Kwanza, ni mvulana mdogo kwenye kiti cha kusukumia wagonjwa.

Tunaweka mikono juu ya mtoto huyu, katika Jina la Yesu Kristo, apate kuponywa.

Naam, bwana.

Katika Jina la Yesu Kristo . . . [Ndugu Branham na wahudumu wanaweka mikono juu ya wale walio kwenye mstari wa maombi, lakini maombi hayasikiki. Kusanyiko linaomba na kuendelea kuimba *Ni Tabibu wa Karibu.*—Mh.]

Pweke limetukuka,
Jina Lake Yesu.

176 Ni wangapi wenu wanaoamini ya kwamba Mungu amejibu, una hakika katika moyo wako, kwa hakikisho lililotiwa muhuri, ya kwamba Mungu ameyajibu maombi yako kwa sababu wewe umelitii Neno Lake? Imetendeka. Imekwisha. I—imekamilika. Mwamini Yeye kwa moyo wako wote, ya kwamba ni kazi iliyomalizika.

177 Sasa angalia juma hili, na utakaporudi tena, angalia yaliyotukia.

178 Ninafikiri, mnamo wakati ule mwingine nitakaporudi, Bwana akipenda, nitakuwa nikipitisha mstari wa maombi kwenye moja ya vyumba hivi, kwenye kile chumba kidogo nitakachowapeleka, mnaona. Ninaamini linajidhihirisha sasa, mnaona, ile saa.

179 Ninataka kufikia mahali ninapoweza kuwaleta watu mmoja kwa zamu, niwashughulikie kibinafsi, mpaka nitafute kabisa hicho na nikipate, halafu niendelee namna hiyo, mpaka nikae moja kwa moja nao wakati huo.

180 Mungu awabariki ninyi nyote. Tunafurahi sana ya kwamba mlikuwa hapa. Je! mmeninii . . . Mmeng'ang'ania sasa? Je! mnaninii . . . Mmekata tamaa, kukata tamaa mlikokuwa nako

kwa ajili ya kuponywa kwenu? Je! kote kumekoma sasa, katika upendo na imani na ujasiri ya kwamba Mungu atafanya kile alichoahidi kufanya? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mungu atafanya.

Kutoka kwa hao watoto wadogo, kuna wawili ama watatu hapa usiku wa leo, katika viti vya kusukumia wagonjwa, mimi. . . .Tutaamini kwa ajili yao, wao ni watoto, kwamba wataponywa, pia. Watapata afya. Hivi hamwaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina.—Mh.] Amina! "Watapata afya." Hawana budi kupona. Mungu alisema hivyo. Nasi tumekata tamaa, na tutaamini jambo hilo sasa, ya kwamba litatimizwa.

181 Sasa, ibada zetu zinahusisha jambo moja baada ya lingine. Sasa tutaacha wasikilizaji wafumukane kwa ajili ya hao wanaopaswa kuondoka. Na niwezavyo kuona, ni kama saa nne kasoro dakika nane. Na, kama itawabidi kuondoka, tu—tuna furaha mlikuwa hapa, nasi tunawataka mrudi mwe pamoja nasi. Ninyi wengine, baada ya sisi kusimama, mtaketi tena; na hao wanaoondoka, mwondoke kwa utulivu mwezavyo. Na halafu basi tutakuwa na ibada ya ushirika mara baadaye. Unaalikwa kukaa ukiweza. Kama huwezi, Mungu akubariki. Niombeeni. Nitawaombea. Pia, kumbukeni, ipakeni ile Ishara wakati wote, na mkate tamaa na kujiingiza kwa nguvu katika Ufalme wa Mungu. Amina!

Sasa, tutaimba wimbo wetu wa kufumukana, tukiweza, na, *Peleka Jina la Yesu*, tunaposimama.

> . . .Jina la Yesu,
> Po pote uendapo;
> Litafurahisha moyo,
> . . .uendako.
>
> Thamani, thamani, na tamu! na tamu!
> Ni Jina Lake Yesu;
> Thamani, na tamu! na tamu!
> Ni Jina Lake Yesu.

Peaneni mikono ninyi kwa ninyi, mseme, "Bwana akubariki, ndugu msafiri, dada." Moyoni, kwa dhati, kwa uchaji, na marafiki Wakristo katika vifungo vya ushirika, peaneni mikono, ndugu na dada. Mungu awabariki nyote, pamoja. Ni ajabu sana!

> Ninampenda, ninampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.
>
> Hata twonane huko juu,
> Hata twonane Kwake kwema; Kwake kwema!
> Hata twonane huko juu,
> Mungu awe nanyi daima.

Hata twonane huko juu,
Hata twonane Kwake kwema; Kwake kwema!
Hata twonane huko juu,
Mungu awe nanyi daima.

[Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Mungu Awe Nanyi Daima*.—Mh.]

182 Utamu huu wa ushirika wa ile Ishara kuu ya Mungu, Roho Mtakatifu, naomba akae ndani yenu nyote kwa wingi mpaka tutakapokutana tena. Neema ya Mungu na iende pamoja nanyi, azipige njia za mauti mbele zenu; akizifanya njia zenu nyeupe, mpate kumwona Yesu daima mbele za uso wenu, wala hamtatikiswa.

183 Baba wa Mbinguni, tunaiweka ibada hii, na ibada ya asubuhi ya leo, ibada hizo na yale yaliyofanywa, na utukufu wote uwe Kwako, tukikushukuru na kukutukuza kwa kuwaokoa watu, na kwa kuwaponya watu, na kwa kutupa neema Yako kuu ambayo sote tunaitazamia. Tuokoe. Jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya jambo hili. Uwe pamoja nasi sasa hata tutakapokutana tena. Kutana nasi katika ushirika. Uwe kwenye gurudumu ya wale wanaoendesha magari, Bwana, wakienda zao nyumbani kwao. Waongoze katika likizo hizi zenye hatari, ili kwamba wasipatwe na madhara yo yote wala hatari. Katika Jina la Yesu Kristo tunaomba. Amina.

Vema, *Peleka Jina La Yesu*, tena sasa.

Peleka . . . Jina la . . . (Mnaweza kuondoka sasa,
katika Jina la) . . . Yesu,
Liwe silaha yako;
Utakapojaribiwa . . .

Ufanye nini basi?

Lilia Jina hilo.

Thamani, thamani! na tamu! na tamu!
Ni Jina Lake Yesu.
Thamani, dhamani! na tamu! na tamu!
Ni Jina Lake Yesu.

Katika Jina la Yesu,
Nimejiinamisha;
Ndiye Mfalme wa wafalme,
Hakika ya maisha.

Thamani, na tamu!
Ni Jina Lake Yesu.
Thamani, na tamu! na tamu!
Ni Jina Lake Yesu.

184 Sasa kabla tu hamjaketi chini, wakati kusanyiko linapotulia sasa kwa ajili ya ibada ya ushirika.

Kama sijakosea, huyu siye Ndugu Blair, yule mhudumu niliyekutana naye kule Arkansas si muda mrefu uliopita?

Nilifikiri alikuwa ndiye. Sikuwa na hakika. Ulikuwa hapa na mtoto wa kuwekwa wakfu, mtoto mchanga, asubuhi ya leo. Nikawazia . . . Hivi sikukutana nawe muda mrefu uliopita, hapa Hot Springs, Arkansas? Ulikuwa na ninii . . . Jambo fulani lilikuwa karibu kutukia, na Roho Mtkatifu akalinena. Hilo lilikuwa ni kweli? Vizuri. Nilininii tu . . . Ilitokea kwamba nilikumbuka jambo hilo basi, nikawazia, “Huyo ni yule ndugu.” Nina furaha sana uko hapa, Ndugu Blair.

185 Sasa nitamwomba Ndugu Blair kama atamwomba Mungu atusafishe sasa kwa ajili ya ushirika ambao uko karibu kuanza. Utatuongoza tafadhali, Ndugu Blair? [Ndugu Blair anaomba—Mh.] Ndiyo. Ndiyo, Bwana. Tujalie, Bwana. Ndiyo, Bwana. Ndiyo, Bwana. Ndiyo, Bwana. Ndiyo. Ndiyo. Amina.

Mnaweza kuketi sasa, kila mmoja.

186 Na sasa kwenye kinanda, dada, kama ninyi nyote chezeni *Damu Imebubujika* tafadhali. Na mnaweza kuanza ninii yenu . . . pelekeni kule, cho chote kinachohitajika. Vema, tusome sasa, kama sote tukiwa tu . . . tukitulia kwa muda mfupi tu.

Ndiyo, dada? [Dada mmoja anasema, “Nichukue kitambaa changu?”—Mh.] Sawa, dada, angalia tu hapa pote mpaka ukipate, itakuwa sawa basi, po pote kilipo. Ndicho hicho? Vema, dada.

187 Vema, sasa Ndugu Neville atasoma utaratibu wa ushirika.

Halafu mabawabu watakuja, kama kuna wageni hapa, kwenye kila kiti, na walete marefu ya kanisa kwa marefu ya kanisa, tunapokuja, na safu kwa safu kwa ajili ya ushirika.

188 Na sasa, mnaombwa kutafakari sasa. Kumbukeni, Israeli waliula katika kukata tamaa, na kote safarini hapakuwepo na mtu mnyonge hata mmoja kati yao, mwishoni mwa miaka arobaini. Huu ni uponyaji wa Kiungu, pia.

Bwana akubariki, Ndugu Neville. [Ndugu Neville anasoma Maandiko yafuatayo, Wakorintho wa Kwanza 11:23-32.—Mh.]

> *Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa nanyi, ya kuwa Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate,*
>
> *Naye akiisha kushukuru akaumega, akasema, Twaeni, mle: huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.*
>
> *Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, Kikombe hiki ni agano Jipya katika damu yangu; fanyeni hivi, kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu.*
>
> *Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo.*

Basi kila aulaye mkate huu, na kukinywea kikombe hiki cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana.

Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe.

Maana alaye na kunywa isivyostahili, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili.

Kwa sababu hiyo wako wengi kwenu walio hawawezi na dhaifu, na watu kadha wa kadha wamelala.

Lakini kama tungejipambanua nafsi zetu, tusingehukumiwa.

Ila tuhukumiwapo, twarudiwa na Bwana, isije ikatupasa adhabu pamoja na dunia.

[Ndugu Neville anasema, "Bwana na abariki hilo somo, Neno." Ndugu Branham basi anachukua sinia la mkate uliovunjwa.—Mh.]

189 Ninashika mkate wa kosha, ulio na makunyanzi na umevunjwavunjwa, unaowakilisha Mwili wa Yesu Kristo; kupitia—kupitia katika pazia hili lililopasuliwa tuna ruhusa ya kuingia katika Patakatifu pa patakatifu.

190 Baba yetu wa Mbinguni, mkate huu umetayarishwa kuwakilisha huo mwili uliovunjwa na kuraruliwa. Jalia kila mmoja wetu, tunavyoupokea, na iwe kama kwamba tulifanya kitendo hiki dhahiri. Na jalia tupate msamaha wa dhambi zetu, na ruhusa ya kuingia katika Patakatifu pa patakatifu, kuishi katika Uwepo Wako katika maisha yetu ya baadaye; na siku zote ambazo tutaishi hapa duniani, na tuwe pamoja Nawe katika Umilele milele. Tujalie, Baba. Ubariki mkate huu kwa matumizi uliyokusudiwa. Katika Jina la Yesu. Amina.

191 [Ndugu Branham anachukua sinia la glasi ndogo zilizojaa divai—Mh.] Biblia ilisema, "Na Baada ya kuutwaa na kuuvunja mkate, vivi hivi akakitwaa kikombe, na akiisha kunywaa, akasema, 'Kikombe hiki ni kikombe cha Agano Jipya katika Damu Yangu, ambayo inamwagwa kwa ajili yenu.'" Bwana na atujalie baraka Zake kwa jambo hili tunapoomba.

192 Bwana Yesu, ninashika hapa damu ya mzabibu, maji ya zabibu. Na, Baba, ni ya kuwakilisha ile Damu ya thamani inayotuosha, kwamba kutoka Humo ikaja ile Ishara. Ninakushukuru kwa ajili Yake, Baba, na kwa ajili ya mfano huu. Ulisema, "Yeye alaye Huu na kuinywa Hii yuna Uzima wa milele, nami nitamfufua tena wakati wa mwisho." Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya ahadi hii. Na, Baba, tunaomba ya kwamba Wewe utaisafisha mioyo yetu, pamoja, tupate kustahili kwa ninii . . . imani yetu; tukijua ya kwamba ndani yetu sisi wenyewe hatustahili, lakini imani yetu haitashindwa, ya kwamba

tunakubali kikamilifu Damu ya Yesu Kristo. Tujalie haya, Baba.

193 Pia itakase divai kwa matumizi iliyokusudiwa. Naomba kila ainywaye divai hii usiku wa leo, na kuula mkate huu, apate nguvu kwa ajili ya safari iliyo mbele. Tujalie, Bwana. Naomba wawe na afya njema na wenye nguvu, na wajazwe na Roho Wako, mpaka Yesu atakapokuja. Amina.

Kukata Tamaa SWA63-0901E
(Desperations)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, tarehe 1 Septemba, 1963, katika Maskani ya Branham, huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1999 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org